
SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Saratani** shingo ya kizazi tishio kwa wanawake

UKURASA 7




# Nipashe

Jumatatu Machi 21, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580891

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


**WACHEZAJI WA5 WALIOKO KWENYE KLABU ISIYO SAHIHI**

UKURASA 12 & 13



# Mbowe aeleza mambo manne aliyoteta na Samia

• **ACT:** Katiba Mpya, tume huru havitenganishiki... *Ukurasa 2*



Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis (kulia), akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa EATV, Regina Mengi wakitembelea maonyesho ya bidhaa mbalimbali katika kilele cha Mwanamke Kinara, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **Picha zaidi ukurasa 8. PICHA: MIRAJI MSALA**

## EATV yampa tuzo Samia uongozi bora

UKURASA 3

# Serikali yafungua fursa ya uwekezaji nishati

UKURASA 3

**MICHEZO** **MOALLIN AANZA KUONA MWANGA AZAM FC** UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6




Kamishna wa Tume ya Madini, Janet Reuben (kulia), akimkabidhi cheti Mwenyekiti wa Wings Youth Group, Yusuph Gesase, katika mahafali ya programu ya kuendeleza biashara za ndani ya kampuni ya Barrick North Mara iliyofanyika Mwanza mwishoni mwa wiki. Wengine ni Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Kanali Michael Mtenjele (watatu kulia), Meneja wa Ukaguzi wa Fedha, Kodi na Ushirikishwaji wa Watanzania wa Tume ya Madini, Geoffrey Nsemwa na Meneja wa Uhusiano kwa Jamii wa Barrick North Mara, Gilbert Mworia (kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbowe adokeza mambo manne aliyoteta na Samia

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amedokeza mambo manne aliyoteta Ikulu na Rais Samia Suluhu Hassan, baada ya kufutiwa mashtaka yaliyokuwa yakimkabili na wenzake watatu.

Akizungumza jana na mamia ya waumini na wafuasi wa chama chake waliomsindikiza kushiriki ibada ya shukrani katika Usharika wa Nshara, Dayosisi ya Kaskazini Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Mbowe alisema, licha ya tukio hilo kubwa alilopitia, hajutii, kwa sababu Mungu ana makusudi na kila jambo.

"Kikao cha kwanza, baada ya gerezani nilikwenda Ikulu, nikamwambia Mheshimiwa Rais (Samia), hii nchi kuna watu wanavuja mioyo yao damu.

"Na nikamwambia Mheshimiwa Rais, hofu inayojengwa na wasaidizi wa watawala, kwamba wana CHADEMA wanavurugu, hawapendi amani ya nchi hii, ni maneno ya uongo.

"Hayajawahi kuwa matamanio au maombi yetu, washindwe kutekeleza vizuri majukumu yao. Tunawaombea wafanye kazi yao kwa uadilifu, wafanye kazi yao kwa haki, nchi yetu ipate ustawi.

"Ustawi wa taifa hili ukipatikana, wawe ni wana CHADEMA, wawe hawana chama, utaona maisha bora kwa kila Mtanzania. Hili ndiyo jambo ambalo CHADEMA tunalihubiri."

Machi 4, mwaka huu, Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP), aliwasilisha mahakamani hati ya kutokuwa na nia ya kuendelea na kesi hiyo iliyokuwa inamkabili katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi.

Katika salamu zake, Mbowe, alisema suala lingine alilozungumza na Rais Samia ni kuhusu chama chake kinapopishana na serikali yake ni (CHADEMA) wanapohubiri haki, wao wanahubiri amani.

"Tulikubaliana kwamba wote tukutane kwenye neno haki, tubadilishe mazoea ya viongozi wa nchi yetu kuhubiri haki. Viongozi wa dini, samahani! Wanahubiri amani amani! Na wanahubiri amani wakijua kwamba uchaguzi haukuwa huru na haki.

"Wanahubiri amani wakati wanajua kuna watu wanateswa, wanahubiri amani wakijua wanafungwa watu kwa makosa. Wakihubiri amani wakati wanajua nchi hii kuna ubaguzi, tutoke hapo kwenye hayo maneno amani. Tuzungumze wote haki; wa chama chochote cha siasa waitangulize haki ya taifa, haki ya raia, haki ya wananchi na kila haki ina wajibu wake. Lakini ni dhahiri tukikubaliana tunakutana kwenye haki, wala hatutagombana."

Pia Mbowe, alisema alimshauri Rais Samia, kuendesha serikali kwa misingi ya haki na CHADEMA, ambacho ni chama kikuu cha upinzani, kuendelea kuhubiri demokrasia na misingi yake yote hadi siku Mungu atawapa kibali waje waiongoze serikali.

"Nikamwambia Mheshimiwa Rais, tumekibaliana kwenye hilo, akaniambia tunakubaliana. Nikasema kama tunakubaliana ni jambo jema, na mimi nimelizungumza chini ya paa la nyumba ya Bwana.

"Nikamwambia, tukatoe kauli yetu mbele ya dunia, uzungumze na mimi nizungumze kwamba wewe kama Rais wa nchi, ndiyo kiongozi wa chama kinachoongoza taifa na sio chama kinachotawala. Na mimi kama kiongozi wa chama kikuu cha upinzani, tukazungumze na dunia, tuweke kauli na kila mmoja asimame kwenye kauli hii na dunia ione.

"Kama sisi tutakuwa wa kwanza kuvunja agano hilo, dunia itasema. Kama wao watakuwa wa kwanza kulivunja agano hilo, dunia itasema. Kwa hiyo huo ndiyo msingi na wakati wote tunapozungumza neno haki, yawezekana haki ikawa ni tafsiri ya mtu. Wewe unaona jambo ni haki, mwenzako anaona sio haki."

"Ili taifa liweze kusimama kwenye haki, lazima liunganishwe. Tunaliunganisha hili taifa na nini? Lazima sheria za nchi zinazoongoza taifa ziwe zina maridhiano. Maana yake mimi naweza nikatoka Ikulu na mtazamo wangu wa haki, naye akabaki na mtazamo wake wa haki. Tayari tumeshapishana.

"Lakini pale watu wanapozungumza na tukakubaliana kama taifa ni nini haki za wakulima, ni nini haki za wafanyabiashara wetu, ni nini haki za watoto wetu? Haki kwa makundi yote, haki hata katika kuwapata viongozi wa kuliongoza taifa letu, haki katika uchaguzi, ugomvi katika mataifa unazaliwa kwenye uchaguzi."

Mbowe alisema, ameweka nadhiri ya kutafuta popote, Sh. milioni 100 za kujenga madhabahu ya Bwana, kwa kuwa anahitaji kuacha alama ya kudumu ili kila atakayefika Kanisa la Nshara la KKKT, akiangalia aseme ni kumbukumbu ya miezi minane ya Mbowe gerezani.

# ACT: Katiba mpya, tume huru havitenganishiki

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kutokana na mazingira ya kisiasa yaliyoko sasa yanapaswa kuendana na upatikanaji wa tume huru ya uchaguzi pamoja na Katiba Mpya yenye maoni ya wananchi, masuala ambayo hayatenganishiki na yanategemeana.

Mwenyekiti wa chama hicho taifa, Juma Duni Haji, alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza na wanachama na viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam, kwenye uzinduzi wa Operesheni ya Tume Huru ya Uchaguzi, ikiwa ni mara yake ya kwanza tangu alipochaguliwa kushika nafasi hiyo akirithi mikoba ya Hayati Maalim Seif Sharif Hamad.

"Malengo ya operesheni hii ni kuhakikisha kuwa tunamfikia kila mwanachama, kiongozi na mwananchi na kuwaelimisha kuwa mazingira yetu ya kisiasa tunapaswa kuipata tume huru ya uchaguzi kuelekea kuipata Katiba Mpya.

"Sote ni mashahidi wa machungu ambayo tumeyapitia. Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2019 na Uchaguzi Mkuu mwaka 2020 umetuachia makovu yasiyo na mfano, ambayo hayawezi kufutika kwa urahisi.

"Wagombea wengi wenye sifa walienguliwa na wale waliopenya katika dirisha la uteuzi, waliporwa ushindi wao," alisema Duni.

Duni alisema chama hicho, kilichukua jukumu la kumwandikia barua rais, Mei mwaka jana, kupendekeza masuala mbalimbali ya kufanyiwa kazi ili kufungua ukurasa mpya wa kisiasa nchini.

"Kwenye barua yetu, iliyoandikwa na Kiongozi wa Chama, Zitto Kabwe, tulipendekeza kwa Rais Katiba Mpya, Tume ya Uchaguzi, Mageuzi ya Jeshi la Polisi na kuandikwa upya kwa Sheria ya Vyama vya Siasa.

Duni alisema chama hicho kinaamini kuwa tume huru ya uchaguzi na Katiba Mpya kutokana na maoni ya wananchi yaliyokusanywa, kuchambuliwa na kuwasilishwa na Tume ya Jaji Warioba.

"Tunahitaji kuandaa na kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2024, ambao kwa muda uliobaki ni bayana kuwa utafanyika kabla hatujawa na hakika ya Katiba Mpya. Pia kuandaa na kusimamia Uchaguzi Mkuu ujao wa mwaka 2025, iwapo utafanyika kabla ya kupatikana kwa Katiba Mpya," alibainisha Duni.

Aliongeza kwamba tume huru ya uchaguzi, iwe angalau na theluthi ya wajumbe wa kamati wa kuteuliwa wawe wanawake. Isiyo na makada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), akisema iliyo na viongozi, wajumbe na watendaji wataopatikana kwa mchakato wa wazi, huru na shindanishi.

"Tunapendekeza kuunda Sheria mpya ya Uchaguzi ya mwaka 2022, itakayoweka utaratibu kuwa Watanzania wanaotaka kuwa Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi waombe kazi kufuatia tangazo la wazi kwa umma," alisema Duni.

"Wasimamizi wa uchaguzi na watendaji wa tume kutoka ngazi ya taifa, majimbo, kata hadi ngazi za chini wawe waajiriwa wa tume kwa utaratibu wa wazi na kwa kuzingatia sifa na vigezo vya uwezo na weledi."

HABARI KITAIFA

# Serikali yafungua fursa uwekezaji nishati

**Na Pascal Mayalla**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amesema moja ya changamoto kubwa katika umeme nchini ni uwekezaji usiotosheleza katika sekta ya nishati na kwamba katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan, amefungua nchi katika fursa za uwekezaji. Vile vile, Waziri Makamba amesema lengo ni kurudisha imani kwa nchi tajiri na wawekezaji wakubwa kuja kuwekeza Tanzania na kufungua milango uwekezaji kwenye nishati. Waziri Makamba, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza kwenye kipindi cha "Kwa Maslahi ya Taifa."

Alisema: "Kwa nchi yenye ukubwa kama wa nchi yetu, na inayokuwa kwa kasi kama yetu, na ongezeko la idadi ya watu, hadi kufikia watu milioni 60, kuwa na Megawati 1,600 ni aibu kubwa, au kuwa na mtandao mdogo wa usafirishaji umeme kama tulionao ni aibu."

Akizungumzia mafanikio ya mwaka mmoja wa Rais Samia madarakani, alisema ni pamoja na kuendelea kuifungua nchi kwa wawekezaji wakubwa na kutolea mfano, kwenye Kongamano la Uwekezaji Sekta ya Nishati, lililofanyika Siku ya Tanzania, kwenye Maonyesho ya Expo Dubai, na kuhudhuriwa na Rais Samia.

"Ttumezungumza na wawekezaji wengi, wakubwa wenye uwezo, na nia njema ambao wako tayari kuja nchini kwetu na kuwekeza katika maeneo hayo," alisema.

Alisema uwapo wa Rais Samia kwenye kongamano hilo, umeleta hamasa ya kipekee kwa kuvutia wawekezaji wakubwa kuhudhuria na kuendelea kufungua milango ya fursa za uwekezaji mkubwa kwa Tanzania. Kuhusu mafanikio kwenye sekta ya nishati, alisema ni pamoja maendeleo ya mradi wa Julius Nyerere (JNHPP) wa kuzalisha umeme, kwenye Stigler Gorge, toka mradi huo umeanza, limejengwa bwawa pekee la kuzalisha umeme, lakini baada ya Rais Samia kuingia, ametoa fedha za ujenzi wa miundombinu ya kuusambaza umeme unaozalishwa, ili ufike kwenye Gridi ya Taifa.

# EATV yampa tuzo Samia uongozi bora

**Na Romana Mallya**

KAMPENI ya Mwanamke Kinara 2022 inayoendeshwa kila mwaka na EATV na East Africa Radio imempa tuzo ya uongozi bora Rais Samia Suluhu Hassan.

Pia, imetoa tuzo kwa Spika wa Bunge, Tulia Ackson na mawaziri wanawake 10 wanaoongoza wizara mbalimbali wakiwamo Waziri wa Ulinzi, Dk. Stergomena Tax na Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Liberata Mulamula.

Wengine ni Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, Waziri wa Nchi Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenister Mhagama na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dorothy Gwajima.

Tuzo hizo pia zimeenda kwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashantu Kijaji, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Pindi Chana.

Katika hafla hiyo iliyofanyika juzi mkoani Dar es Salaam mgeni rasmi alikuwa Naibu Waziri Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalumu, Mwanaidi Ali Khamis, ambaye aliwakabidhi vyeti wanawake 10 ambao washindi wa tuzo ya Mwanamke Kinara2022 kutokana na mambo makubwa wanayofanya ndani ya jamii.

Miongoni mwao ni Jenifer Hadson mwenyeji wa Arusha anayeendesha mashine nzito katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na wengine ambao mikoa yao ipo kwenye mabano ni Dk. Herieth Mkanga (Morogoro), Tabla Makame (Zanzibar), Happiness Mathias (Katavi), Leticia Njunju (Mtwara), Noel Msuya (Mbeya), Foida Kawago, Mariam Elisha na Rita Batholomeo wote kutoka Iringa.

Naibu Waziri, Mwanaidi aliiomba EATV iendelee kuelimisha wanawake kuhusu fursa za mikopo zinazopatikana kupitia halmashauri ili waichangamkie kukuza uchumi wao.

Alisema Rais Samia anasaka wawekezaji ili kukuza uchumi na kuwataka wanawake wasibaki nyuma kuchangamkia fursa mbalimbali zinazotolewa.

Mtangazaji wa kipindi cha DADAZ EATV, Bhoke Egina, alisema kampeni ya Mwanamke Kinara lengo lake ni kumwinua mwanamke kiuchumi kwa kumpatia elimu.

Mkurugenzi wa Biashara TDL, Timea Chogo, alisema kitendo cha Samia kuwa Rais kimefungua milango kwa watoto wa kike ambao sasa ndoto zao ni kushika nafasi kubwa.

Mkuu wa Masoko kutoka Benki ya UBA, Brendansia Kileo, alisema benki yao inatoa mikopo kuanzia asimilia sifuri kuendelea na kuwataka wanawake kuchangamkia ili waweze kukuza biashara zao.

Msaidizi wa Usajili kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Marryglory Mmari, aliwapa elimu wanawake namna wanavyoweza kusajili biashara zao na kampuni ili zitambulike kisheria na kuweza kupata fursa za mikopo.

# Radi yaua ng'ombe zikitoka malishoni

**Na Neema Hussein,** KATAVI

NG'OMBE 28 za wafugaji watano katika kijiji cha Kabage wilayani Tanganyika mkoani Katavi zimepigwa radi wakati zikitoka malishoni.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Maico Kushoka, alisema tukio hilo lilitokea Jumamosi jioni baada ya mvua kunyesha ikiambatana na radi.

Alisema wachungaji hao walikuwa na ng'ombe 42 kati yao 28 zilipigwa radi wakati wakirudi nyumbani kutoka machungani mvua ilipoanza kunyesha.

"Waliona mwanga wa radi wakatawanyika baadaye waliona ng'ombe mmoja amekufa, wakaenda kutoa taarifa nyumbani," alisema Kushoka.

Alisema baada ya kurudi waliona zingine 27 zimekufa, ng'ombe tisa zilikuwa mali ya Sitta Busheneli, Mwanamazuri ng'ombe 8, Masanja 5, Makune 4 na wawili hazikutambulika mmliki.

Aidha, alisema kiongozi wa kimila alifika eneo hilo kufanya tambiko la kimila kisha wananchi walichinja na kugawana kitoweo.

Alisema tukio hilo la pili kutokea mwaka 2018 zilikufa ng'ombe nne kwa kupigwa radi, lakini tukio la jana nyumba tatu zilibomoka na barabara imekatika, lakini hakukuwa na madhara kwa binadamu.

Sitta Busheneli ambaye ng'ombe zake 9 zilpigwa radi, alisema alipokea taarifa hizo kwa masikitiko makubwa na kwamba kitendo hicho kimemrudisha nyuma kimaendeleo.




**KUPOTEA KWA KWA KADI YA GARI**

ROTARY CLUB OF ARUSHA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya MASSEY FERGUSON yenye namba za usajili T 633 AQJ,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa

ARU/ARU/RB/112358/2022

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**OSWARD TOMU MWAMFUPI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA COASTER yenye namba za usajili **T 893 DGR,** Engine No: **1HD510001168,** Chassis No: **HDB510001168,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa

**DSM/PHQ/RB/110264/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO**
**Unapojibu tafadhali taja:**
**Kumb.Na: MMC/LD/15339**
**Tarehe: 11.03.2022**
**MUSTAPHA RAMADHANI,**
**S.L.P 217,**
**MOROGORO.**
**YAH: NIA YA KUTOHUISHA MILIKI YA KIWANJA NA. 128 KITALU"B" MSAMVU**

Rejea kichwa cha habari hapo juu.

Kiwanja Na.128 Kitalu B Msamvu hapo awali kilitolewa kwa ndugu Mustafa Ramadhani kupitia Hati Na. 35881 iliyotolewa muda wa miaka 33 kuanzia tarehe01/01/1988 kwa matumizi ya makazi miliki hiyo ilikwisha muda wake tangu tarehe 30/12/2021.Aidha mwaka 1998 ilitolewa pia Barua toleo (Ofa) kwa Ndugu Macmillan S. Moshy ambaye ameendeleza kwa kujenga nyumba ya makazi.

Kupitia fungu la 32 la sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 Ofisi haina nia ya kuendelea kuhuisha milki ya Ndg Mustafa Ramadhani kwani alishindwa kuendeleza kiwanja hicho kwa kufuata kanuni na taratibu.

Aidha tunakusudia kumilikisha milki hii kwa Ndg Macmillan S.Moshy ambaye mpaka sasa ndiye ameendeleza kiwanja hicho.

Hivyo mtu yeyote mwenye pingamizi au maslahi juu ya kiwanja hiki anatakiwa kutoa taarifa kwa Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Morogoro S.L.P 587 Morogoro ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya barua hii.

VALENCY H.K
K.N.Y MKURUGENZI WA MANISPAA
MOROGORO

## SHIRIKA LA UMEME TANZANIA



### TAARIFA YA MAFANIKIO YA TANESCO KWA KIPINDI CHA MWAKA MMOJA WA UONGOZI WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA AWAMU YA SITA MHE. SAMIA SULUHU HASSAN

# TAARIFA YA MAFANIKIO YA TANESCO KATIKA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KIPINDI CHA MWAKA MMOJA MARCH 2021 HADI MARCH 2022.



**Mhe. Samia Suluhu Hassan**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**Utangulizi**

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lilianzishwa mwaka 1964 kwa kuunganisha mashirika binafsi mawili ya Tanganyika Electric Supply Company Limited (TANESCO) na Dar es Salaam and District Electric Supply Company Limited (DARESCO) chini ya sheria ya umeme ya mwaka 1931 iliyorekebishwa mwaka 1957 (Electricity Ordinance Cap 131 of 1931, na maboresho ya mwaka 1957). Kuanzia Mwaka 1968 Serikali ilianza kununua hisa za TANESCO na hadi kufikia mwaka 1975 hisa zote zilikuwa chini ya Serikali, hivyo kuifanya kuwa Shirika la Umma ambalo linamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100. Baada ya kupata Uhuru mnamo mwaka 1961, TANESCO ilianza kupanga mikakati ya kupata miradi mipya ya kuzalisha umeme na kujenga njia za kusafirisha na kusambaza umeme kwa viwanda na miji nchini kote. Tafiti za kufua umeme wa maji zilianza ili kupunguza gharama za kufua umeme wa mafuta kutoka nje.

**MAFANIKIO YA JUMLA**

Shirika limekuwa na mafanikio mbalimbali yaliyotokana na mchango mkubwa wa Serikali kupitia Wizara ya Nishati katika utekelezaji wa majukumu yake.

**Mafanikio ambayo TANESCO imeyapata ni pamoja na:**

1. Ongezeko la miundo mbinu ya kusafirisha na kusambaza umeme. kilometa 6,110.57 za usafirishaji umeme, ambapo kilometa 670 ni za msongo wa 400kV, kilometa 3,225 ni za msongo wa 220kV, kilometa 1,672.57 ni za msongo wa 132kV na kilometa 543 ni za msongo wa 66kV.

Vile vile urefu wa njia za usambazaji umeme umeongezeka na kufikia kilomita 47,487.88 za msongo wa kilovoti 33, kilometa 12,486.11 za msongo wa kilovoti 11 na kilometa 88,570.24 za msongo wa chini (400V/231V).

2. Shirika limeimarisha hali ya upatikanaji wa umeme nchini ambapo hadi kufikia mwezi Disemba 2021 jumla ya uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme iliyounganishwa katika Gridi kuu ya Taifa imefikia MW 1,573.65 kati ya hizo MW 573.70 zinatokana na vyanzo vya maji, MW 901.32 gesi asilia na MW 10.50 tungamotaka (Biomass). Uwezo wa mitambo ya kufua umeme inajumuisha mitambo inayomilikiwa na TANESCO ambayo huchangia asilimia 86.57 na mitambo ya wazalishaji binafsi (IPP/SPPs) ambayo huchangia asilimia 13.43. Vile vile TANESCO inamiliki mitambo ambayo haijaunganishwa katika mfumo wa Gridi kuu ya Taifa yenye uwezo wa kuzalisha MW 32.21 na hivyo kufanya jumla ya uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme nchini kufikia MW 1,605.86. Mitambo hii inaweza kukidhi mahitaji ya juu ya umeme ambayo yameendelea kuongezeka na kufikia MW 1,307.36 mwezi November 2021.

TANESCO inaendelea na utekelezaji wa miradi mbali mbali ya kufua umeme ili ifikapo mwaka 2025 uwezo wa ufuaji umeme uongezeke na kufikia MW 5,000, na Mwaka 2044 itafikia MW 18,000.

3. Hadi kufika mwezi februari mwaka wa fedha wa 2021/22 idadi ya wateja wa umeme imeongezeka na kufikia 3,655,534 kutoka 3,290,490 kwa mwaka wa fedha 2020/21 sawa na ongezekeo la asilimia 90%. Idadi ya wateja waliounganishiwa umeme (connection level) sasa ni 37.7% ya wananchi wote, na idadi ya wananchi waliofikiwa na huduma ya umeme (access level) ni 78.4%.

4. Shirika limekamilisha ujenzi wa Mradi wa Njia ya kusafirisha umeme kwa ajili ya kuendesha Treni ya Kisasa ya Mwendokasi ya kutumia umeme (Standard Gauge Railway – SGR) Awamu ya Kwanza yenye urefu wa kilomita 160 kutoka Dar es Salaam hadi Kingolwira, Morogoro kwa asilimia 100. Kukamilika kwa mradi huu kutaifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki zinazotumia treni ya kisasa ya mwendokasi yenye kutumia umeme.

Pia Shirkia limeanza ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 410 kutoka Msamvu-Morogoro hadi Kintinku-Singida kwa ajili ya matumizi ya treni ya umeme (SGR awamu ya pili) ambapo hadi sasa umefikia asilimia 85.

5. Shirika linaendelea kukamilisha Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu – Mzunguko wa Kwanza (REA III – Round I) unaolenga kupeleka umeme katika vijiji 3,559 na kuunganisha wateja wa awali 180,768 na kupeleka umeme katika vitongoji 419 ambavyo vina Taasisi zinazotoa huduma kwa jamii zikiwemo Taasisi za Afya na Elimu ndani ya vijiji vilivyofikiwa na umeme, na hivyo kupelekea wateja wa awali kuongezeka hadi kufikia 227,561. Gharama ya mradi ni Shilingi trilioni 1.157. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 jumla ya vijiji 3,378 kati ya 3,559 sawa na asilimia 94.9 na vitongoji 317 kati ya 419 sawa na asilimia 75.7 vilipelekewa umeme na kuunganisha jumla ya wateja 162,198 kati ya 227,561 sawa na asilimia 71.3.

Shirika linaendelea na utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ya kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme kama ilivyoainishwa katika bajeti ya mwaka 2021/22. Katika utekelezaji wa miradi hiyo, Shirika hutegemea vyanzo vikuu viwili vya fedha ambavyo ni fedha kutoka Serikalini zikijumuisha fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na fedha zitokanazo na mapato ya ndani ya Shirika.

Katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo mbalimbali imetenga jumla ya Shilingi trilioni 1.911 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali kupitia TANESCO ikiwemo Julius Nyerere Hydro Power Project (MW 2,115), Ruhudji (MW 358), Rumakali (MW 222), Kinyerezi I Extension (MW 185), kV 400 Julius Nyerere – Dodoma na Kinyerezi kupitia Chalinze, kV 400 Singida – Arusha – Namanga, kV 400 Nyakanazi – Kigoma, kV 220 Rusumo – Nyakanazi na kV 220 Geita - Nyakanazi. Kati ya fedha hizo Shilingi trilioni 1.793 ni fedha za Serikali na Shilingi bilioni 118 ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Utekelezaji wa miradi ya kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme nchini inayotekelezwa na Serikali kupitia TANESCO imefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo:

**A: MIRADI YA KUFUA UMEME INAYOENDELEA KUTEKELEZWA**

*i. Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere – MW 2,115*

Mradi huu unahusu ujenzi wa kufua umeme kiasi cha MW 2,115 kwa kutumia maporomko ya maji ya mto Rufiji. Gharama ya mradi huu ni Shilingi trilioni 6.55 ambazo zinatolewa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100.

Hadi kufikia mwezi Januari, 2022 kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilisha uchimbaji na ujenzi wa handaki la kuchepusha maji ya mto Rufiji (diversion tunnel), kuendelea na ujenzi wa bwawa (main dam and spillways), ujenzi wa njia kuu za kupitisha maji (tunnels), ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme (Power House) na ujenzi wa kituo cha kusafirisha umeme (Switchyard). Utekelezaji wa mradi katika maeneo yote kwa ujumla kimkataba umefikia asilimia 53.25.

*ii. Mradi wa Kufua Umeme wa Rusumo – MW 80*

Mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 80 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Kagera na unahusisha nchi tatu (3) za Tanzania, Burundi na Rwanda kwa mgawanyo sawa kwa kila nchi. Gharama za mradi wa kuzalisha umeme kwa upande wa Tanzania ni Dola za Marekani milioni 113.

Hadi kufikia mwezi Januari, 2022, ujenzi wa eneo la kusimika mitambo (power house) umekamilika na usimikaji wa mitambo umefikia asilimia 52; kukamilika kwa milango ya kuingiza na kuchepusha maji (spillway and intake gates); na kuendelea na uchimbaji wa handaki la kupitishia maji. Utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia asilimia 86.7 na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2022.

*iii. Mradi wa Kufua Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension – MW* 185

Mradi huu unahusu upanuzi wa kituo cha Kinyerezi I – MW 150 kwa kuongeza mitambo itakayofua MW 185 na hivyo kufanya kituo hicho kufua jumla ya MW 335. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100 kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 188.

Hadi sasa, ujenzi wa misingi ya kufunga mitambo umekamilika; mitambo minne (4) ya kufua umeme ipo tayari katika eneo la mradi huku ufungaji wa mitambo miwili (2) ukiwa umeanza; upanuzi wa kituo cha kupokea umeme umekamilika; na ujenzi wa njia ya kuunganisha kituo cha Kinyerezi II umekamilika. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 84. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2022.

Miradi mingine ya uzalishaji wa umeme iliyo katika hatua za awali ni pamoja na

*i. Mradi wa Kufua Umeme wa Malagarasi – MW 49.5*

Mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 49.5 kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Malagarasi Mkoani Kigoma. Aidha, mradi utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 132 yenye urefu wa kilomita 54.5 kutoka Malagarasi hadi Kidahwe, mkoani Kigoma. Gharama za utekelezaji wa mradi ni Dola za Marekani milioni 144.14 na unatekelezwa kwa ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dola za marekani (USD) Milioni 4.14 na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) Dola za marekani (USD) Milioni 140. Mkataba wa ufadhili wa mradi ulisainiwa mwezi Mei, 2021.

# TANGAZO

*ii. Mradi wa Kufua Umeme Jua wa Shinyanga – MWp 150*

Mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia jua chenye uwezo wa MWp 150 katika eneo la Kishapu mkoani Shinyanga. Mradi huu utakaoanza na uzalishaji wa MWp 50 kwa gharama ya EURO Milioni 43 unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Ufaransa (AFD) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi huu utaenda sambamba na mradi wa kuboresha miundombinu ya Gridi (Grid Modernization) ili kuruhusu Gridi kuweza kubeba umeme wa nishati jadidifu utakaogharimu EURO milioni 87 na hivyo kufanya jumla ya gharama ya mradi kuwa EURO milioni 130. Mkataba kwa ajili ya ufadhili wa mradi huu umesainiwa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na AFD mwezi Julai, 2021.

**B: MIRADI YA KUSAFIRISHA UMEME INAYOENDELEA KUTELELEZWA**

i. Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Kituo cha kufua Umeme Cha Julius Nyerere kwenda Dodoma na Kinyerezi kupitia Chalinze

Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 yenye urefu wa kilomita 598 kutoka kituo cha kufua umeme cha Julius Nyerere kwenda Dodoma na Kinyerezi, Dar es Salaam kupitia Chalinze Mkoa wa Pwani. Mradi pia unahusisha ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Chalinze na Kinyerezi. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 420 na mradi unafadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, Mkandarasi (TBEA) anaendelea na maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kutoka Mkuranga – Kinyerezi hadi Dodoma pamoja na kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi

*ii. Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Singida – Arusha – Namanga*

Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 yenye urefu wa kilomita 414 kutoka Singida hadi Namanga kupitia Arusha. Mradi unahusisha ujenzi wa kituo kipya cha kupoza umeme cha Lemugur katika eneo la Kisongo mkoani Arusha na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Singida na usambazaji wa umeme katika vijiji 19 vilivyo jirani na mkuza wa njia ya umeme kwenye mikoa ya Singida, Manyara na Arusha. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo gharama ya mradi ni Dola za Marekani milioni 258.82.

Hatua iliyofikiwa ya utekelezaji wa mradi huu kwa ujumla ni asilimia 79.3. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Machi, 2018 na unatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2022.

*iii. Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma*

Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma yenye urefu wa kilomita 280, ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Kidahwe Mkoani Kigoma, upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi na usambazaji umeme katika vijiji 18 vilivyopo katika eneo la mradi. Gharama za mradi huu ni Dola za Marekani milioni 187 na zinatolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Exim ya Korea Kusini (EDCF) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

*iv. Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Iringa – Mbeya – Tunduma hadi Sumbawanga*

Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kutoka Iringa kupitia Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga yenye urefu wa kilomita 620. Mradi huu utahusisha pia ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Kisada (Iringa), Iganjo (Mbeya), Tunduma na Sumbawanga. Mradi huu unalenga kuunganisha Gridi ya Taifa na nchi za kusini mwa Afrika kupitia Southern African Power Pool (SAPP). Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 610 ambazo zitatolewa na Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Umoja wa Nchi za Ulaya (EU) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

*v. Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Sumbawanga – Mpanda – Kigoma*

Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kutoka Sumbawanga hadi Kigoma kupitia Mpanda yenye urefu wa kilometa 480. Mradi huu unatarajiwa kugharimu Dola za Marekani milioni 200. Kwa sasa mradi huu unaendelea na taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mtaalam Mshauri wa kuandaa ripoti ya mazingira. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Novemba, 2022 na kukamilika mwezi Oktoba, 2024.

*vi. Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220 ya Geita – Nyakanazi*

Mradi huu unahusu: ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 144 kutoka Geita hadi Nyakanazi; ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Nyakanazi; na kusambaza umeme katika vijiji 32 vinavyopitiwa na mradi maeneo ya Geita hadi Bwanga na Nyakanazi hadi Kakonko. Gharama za utekelezaji wa Mradi huu ni EURO milioni 45.

*vii. Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 Rusumo – Nyakanazi*

Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 94 kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Rusumo hadi Nyakanazi. Gharama za Mradi ni Dola za Marekani milioni 35. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

*viii. Mradi wa Backbone Transmission Investment Project – Awamu ya Pili (BTIP – Phase II)*

Mradi huu ni wa awamu ya pili ambao unalenga kuongeza uwezo (upgrade) wa vituo vinne (4) vya kupoza umeme vya Iringa, Shinyanga, Singida na Dodoma kutoka kV 220 mpaka kV 400. Awamu ya kwanza ya mradi ilihusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 400 kutoka Iringa hadi Shinyanga kupitia Dodoma na Singida wenye urefu wa kilomita 670. Mradi huu ulikamilika mwezi Desemba, 2016 na kwa sasa unaendeshwa kwa msongo wa kV 220. Gharama ya mradi huu ni Dola za Marekani milioni 120.

*ix. Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Mwendo Kasi (Standard Gauge Railway – SGR) Awamu ya Kwanza*

Mradi huu ulihusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 160 kutoka Kinyerezi, Dar es Salaam hadi Kingolwira, Morogoro kwa ajili ya kuendesha Treni ya Mwendokasi (Standard Gauge Railway – SGR) awamu ya kwanza. Aidha, mradi huu ulihusisha upanuzi wa kituo cha kupoza umeme msongo wa kV 220 cha Kinyerezi. Gharama ya mradi huu ni Shilingi bilioni 76.23 na unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia 100.

Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Januari, 2019 na hadi kufikia sasa mradi huu umekamilika kwa asilimia 100.

*x. Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Mwendo Kasi (Standard Gauge Railway – SGR) Awamu ya Pili*

Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 410 kutoka Msamvu, Morogoro hadi Kintinku, Singida kwa ajili ya kuendesha Treni ya Mwendokasi (Standard Gauge Railway – SGR) awamu ya pili. Gharama ya mradi huu ni Shilingi bilioni 164.3 na unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia 100.

Ujenzi wa mradi huu ulianza mwezi Novemba, 2020 na hadi sasa umefikia asilimia 85. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Julai, 2022.

**C: MIRADI YA KUBORESHA MIUNDOMBINU YA USAMBAZAJI UMEME NA KUHUDUMIA WATEJA**

*i. Mradi wa Kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme katika Jiji la Dodoma*

Mradi huu utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 kutoka Zuzu kwenda Msalato na kutoka Zuzu kwenda Kikombo pamoja na ujenzi wa vituo viwili (2) vipya vya kupoza na kusambaza umeme katika maeneo ya Msalato na Ihumwa Jijini Dodoma. Gharama ya mradi ni Dola za Marekani milioni 126.1. Kazi iliyofanyika ni pamoja na kuhuisha Upembuzi Yakinifu. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Machi, 2022 na kukamilika mwezi Septemba, 2023.

*ii. Mradi wa Kujenga Kituo Kipya cha Kupoza Umeme Luguruni chenye Msongo wa kV 220/33*

Mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Luguruni kitakachohusisha ufungaji wa transfoma mbili zenye uwezo wa MVA 90 kila moja. Mradi huu utakuwa na matoleo (outgoing feeders) sita (6) ya msongo wa kV 33 ambayo yataboresha upatikanaji wa umeme katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Gharama ya mradi ni Shilingi bilioni 15.2 na unafadhiliwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100.

Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: ujenzi wa misingi ya transfoma na vifaa vya kudhibiti mfumo wa umeme. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 86. Mradi huu ulianza mwezi Aprili, 2020 na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Aprili 2022.

*iii. Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 132 na Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Dege Beach*

Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 132 yenye urefu wa kilomita 14 kutoka Kibada hadi Dege Beach mkoani Dar es Salaam pamoja na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Dege Beach chenye uwezo wa MVA 60, kV 132/33. Gharama ya mradi ni Shilingi bilioni 26.2 na umefadhiliwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100.

**Mradi huu hadi sasa umekamilika kwa asilimia 100.**

*iv. Kituo cha pamoja cha Miito ya simu*

Shirika limeanzisha kituo cha pamoja cha miito ya simu kitakachokuwa na uwezo wa kupokea simu za wateja kutoka mikoa yote ya Tanzania bara. Kwa sasa kituo hiki kimeanza kutoa huduma kwa mikoa iliyo ndani ya kanda ya mashariki; Kinondoni Kaskazini, Kinondoni Kusini, Temeke, Ilala na Pwani. Uratibu wa kuongeza mikoa ya kanda zilizobaki inaendelea ikianzia na kanda ya nyanda za juu kusini.

Kituo hiki kitachochea weledi wa watoa huduma wetu, kupunguza/kusitisha simu kutopokelewa kwa kuzihamisha kwa mtoa huduma mwengine, kupunguza urasimu na mianya ya utendaji kazi iliyo kinyume na taratibu za utoaji wa huduma bora.

Mradi huu unakwenda sambamba na uanzishwaji wa viunga (Vituo vidogo vya utoaji wa huduma za kiufundi mitaani) kwa lengo la kuhakikisha taarifa iliyowasilishwa na mteja inafanyika ndani ya nusu saa. Watoa huduma wetu kupitia mifumo watakuwa na uwezo wa kutuma taarifamp;.

*v. Mfumo wa simu wa kutoa huduma "Mobile Applications)*

Shirika liko katika hatua za mwisho za kuanzisha mfumo wa utoaji wa huduma ikianza na maombi ya huduma za kuunganishwa kwa umeme. Mfumo huu wa kidijitali utahusisha wateja wenye simu za kisasa na simu za kawaida na hautolazimu mteja kufika ofisini.

Maboresho kupitia mfumo huu yamelenga kufupisha utaratibu wa maombi ya umeme unaomlazimu mteja kufika katika ofisi zetu zaidi ya mara tatu kabla ya kuunganishiwa, kuzuia mianya ya vishoka na kuweka uwazi wa kila hatua iliyofikiwa ya ombi la mteja.

Wadau wengine wa mfumo huu watakuwa ni pamoja na wateja, wakandarasi ambapo taarifa zote zitachakatwa kupitia katika mfumo huu. Kwa sasa mfumo upo tayari kuanza matumizi na wafanyakazi wameanza kupatiwa mafunzo.

*vi. Matumizi ya mita janja*

Matumizi ya "smart meter" ni mafanikio mengine yanayotarajiwa kuanza rasmi mwezi Julai 2022. Kupitia mita hizi mteja umeme utakaonunuliwa na mteja utaingia moja kwa moja katika mita yake bila kubofya kama ilivyo katika mita za sasa. Mita hizi pia zitaliwezesha shirika kuona moja kwa moja kiasi ambacho mteja anakitumia kwa wakati huo. Kupitia mita za sasa, kiwango cha matumizi kinatathminiwa kupitia uwezo wa vifaa anavyotumia mteja sambamba na kiasi anachikinunua.

Faida nyingine ni pamoja na kutambua kama eneo lenye mita husika kama lina umeme, utoaji wa taarifa endapo mita inahujumiwa. Kupitia mita hizi shirika litapunguza kiasi cha umeme kinachopotea.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Stars onyesheni kiwango mechi Kalenda ya Fifa

**KUELEKEA** Kalenda ya Shirikisho la Soka Duniani (Fifa), timu ya Taifa ya Soka ya Tanzania, Taifa Stars, itacheza mechi mbili za kirafiki za kimataifa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumatano wiki hii na Jumanne ya juma lijalo. Tayari Shirikisho la Soka nchini (TFF), limefanya juhudi kubwa kupata timu zitakazocheza na Stars mechi hizo mbili ambazo zote zitakuwa ndani ya Kalenda ya Fifa na zitachezwa kwa mtindo wa ligi, ambazo ni dhidi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati na Sudan.

Taifa Stars itaanza kucheza Jumatano wiki hii dhidi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati na kisha Jumamosi ya Machi 26, Watanzania watashuhudia mechi nyingine kali kati ya Sudan na Jamhuri ya Afrika ya Kati.

Mchezo wa mwisho katika ligi hiyo ya mechi hizo za kimataifa ambazo zote zitakuwa ndani ya Kalenda ya Fifa, utakuwa Jumanne ya wiki ijayo Machi 29, Stars ikihitimisha kwa kuvaana na Sudan.

Tayari Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Kim Poulsen, ameshaita kikosi chake kitakachoundwa na wachezaji 28 kilichotarajiwa kuingia kambini jana kuanza kujiandaa na mechi hizo mbili.

Aidha, Poulisen amesema atazitumia mechi hizo mbili kwa ajili ya kuanza kukiandaa kikosi chake kwa ajili ya michuano ijayo ya kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika, Afcon Juni mwaka huu.

Lakini si hilo tu, kwani inapaswa kutambua kwamba kutokana na mechi hizi kuwapo kwenye Kalenda ya Fifa, endapo Stars itapoteza ama kushinda itaifanya Tanzania kushuka au kupanda kwenye viwango vya Fifa wakati huu ikiwa katika nafasi ya 132 duniani.

Kadhalika, mechi hizi ni muhimu kwa kila mchezaji kuonyesha ubora wake kwani mawakala huitupia jicho wakitafuta nyota watakaowauza nje ya nchi, lakini pia klabu za soka nchini huitumia kuanza kumulika nyota wa kuwasajili katika dirisha lijalo.

Kwa mantiki hiyo, wachezaji wanapaswa kutambua kwamba kinachotakiwa hapo pamoja na kuonyesha viwango vyao ili kujitafutia soko na kuendelea kumshawishi Poulsen kuwaita tena awamu ijayo, lakini ushindi ni muhimu kwa manufaa ya kuipasha Tanzania katika viwango vya Fifa.

Ikumbukwe Jamhuri ya Afrika ya Kati yenyewe ipo nafasi ya 130 katika viwango vya Fifa duniani, hivyo kama Tanzania itashinda itakuwa na nafasi kubwa ya kupanda zaidi kutoka 132 ilipo kwa sasa.

Lakini katika mchezo dhidi ya Sudan inayoshika nafasi ya 133 kwa ubora duniani nyuma ya Tanzania, Taifa Stars endapo itapoteza dhidi yao, hiyo inamaanisha itatoa nafasi kwa Wasudan hao kupanda na kuwashusha.

Hivyo, michezo hizo zina maana kubwa sana kwa Tanzania kimataifa, jambo ambalo wachezaji wanapaswa kupambana vilivyo na si kuingia uwanjani wakizichukulia kama michezo yakujifurahisha tu kwao kwa kuwa si ya kimashindano. Mashabiki wa soka nchini na Watanzania kwa ujumla mbali na kiwango cha timu na mchezaji mmoja mmoja, wanachotaka kukiona katika mechi hizo ni ushindi pia, kwani hilo litasaidia kuendelea kuwajenga utamaduni wakwenda uwanjani kwa wingi kuisapoti Taifa Stars kila inapocheza.

Haitapendeza kuona TFF imeandaa mechi hizo kwa gharama kubwa halafu Watanzania wakipata aibu kwa wachezaji wao kuonyesha kiwango kibovu na kupoteza zote mbili.

Hivyo, tunachotaka kukiona ni ubora wa viwango vya kila mcheza na timu kwa ujumla, lakini vyote hivyo vikihitimishwa kwa ushindi na si vinginevyo. Katika hilo, mashabiki wa soka na Watanzania kwa ujumla hawana budi kujitokeza kwa wingi uwanjani katika michezo hiyo ili kubeba vema jukumu la mchezaji wa 12 uwanjani, jambo ambalo tunaamini linaweza kuwa msaada mkubwa Taifa Stars kushinda michezo hiyo miwili.

Tunaamini kadri Stars itakavyoonyesha ubora na kushinda mechi zake licha ya kuipandisha katika viwango vya Fifa, kutairahisishia TFF kwenye kalenda zijayo za mechi za kimataifa kupata timu ya daraja la juu kirahisi za kuja ama Stars kwenda kucheza nazo mechi ya kirafiki.

Ni utamaduni uliojengenga kwa mataifa mengi yaliyo juu kisoka, kukataa kucheza na nchi zilizopo chini yao kwenye viwango vya Fifa, zikikwepa endapo zikifungwa kuporomoka nafasi zao, hivyo kuna njia ya mkato zaidi ya Stars kushinda kila inapocheza mechi zake ziwe za kirafiki ama kimashindano ili kukwea zaidi na kuirahisishia TFF kwenye mchakato wa kusaka mechi za kirafiki.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Prisons haikusoma alama za nyakati Ligi Kuu

**KWA** misimu kadhaa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara huwa tunashuhudia timu zinazoshuka daraja, lazima moja itakuwa ni ile iliyopanda msimu huo huo, na nyingine zilizopanda miaka michache nyuma.

Hata msimu uliopita ilikuwa hivyo baada ya timu ya Gwambina FC iliyopanda kwa mbwembwe, kushuka daraja msimu wa kwanza tu baada ya kucheza Ligi Kuu.

Ihefu nayo ilikuwa hivyo hivyo misimu miwili iliyopita, ilipanda na kushuka. Hata hivyo, naona inajikongoja sana kwenye Ligi ya Championship na haitoshangaza ikapanda na msimu ujao tukawa nayo kwenye Ligi Kuu kwa mara nyingine.

Kwa mara ya kwanza msimu uliopita, pamoja na Gwambina kushuka, ilishuhudiwa timu zoefu kwenye Ligi Kuu, JKT Tanzania ikishuka daraja. Timu hiyo ambayo sasa ipo Ligi ya Championship, ilipanda msimu wa 2006/07, wakati huo ikiitwa JKT Ruvu, lakini baadaye ilibadilishwa jina na kuitwa JKT Tanzania.

Ni timu inayomilikiwa na Jeshi la Kujenga Taifa, ambayo hata kwenye Championship haiko katika nafasi nzuri sana ambayo unaweza kusema msimu ujao inaweza kurudi.

Msimu huu kuna wasiwasi mkubwa, hata kama kuna timu iliyoanza kucheza msimu huu na kushuka daraja kama ilivyo kawaida, tunaweza kushuhudia timu mbili kongwe kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara zikishuka daraja. Nazizungumzia timu za Prisons na Mtibwa Sugar. Pamoja na kwamba Mtibwa Sugar imekuwa angalau inaonekana kujipapatua, lakini Prisons inatia huruma kwani inashika nafasi ya mwisho kabisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 13 kwa mechi 18 ilizocheza.

Imeshinda mechi tatu, sare nne na kupoteza 11, ikiwa ni rekodi mbovu kwa mara ya kwanza tangu ipande Ligi Kuu katikati ya miaka ya 1990.

Prisons ilitwaa ubingwa wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania mwaka 1999, ikiwa ni mafanikio makubwa zaidi kwenye historia yake ya soka. Ili iweze kutoshuka daraja, au kuepuka kucheza mechi za mchujo, inatakiwa ifanye kazi ya ziada. Na kwa bahati mbaya sana, hata viongozi wa klabu hiyo wameonekana hawajui tatizo ni nini kwenye klabu yao.

Matokeo yake iliona ihame kutoka Uwanja wa Nelson Mandela Sumbawanga mkoani Rukwa, ambao ilikuwa inautumia kama uwanja wake wa nyumbani kwa misimu miwili, ikarejea nyumbani kwao kwa asili Mbeya, ikitumia Uwanja wa Sokoine.

Haikuwa dawa kwao, kwani imeendelea kupoteza, si kwenye Ligi Kuu pekee, bali pia Kombe la FA.

Wengi wanajiuliza, Prisons, timu ambayo miaka yote ina wachezaji wanaocheza kwa kutumia nguvu na wagumu kufungika, inayotoa ushindani mkubwa kwa Klabu za Simba na Yanga, leo imekuwa nyanya, huku ikiwa na karibuni wachezaji wale wale, nini kimewatokea.

Viongozi wa klabu hiyo nadhani hawataki kukubali ukweli kuwa wachezaji wake wengi wamechoka.

Ukiiangalia Prisons, ni moja kati ya timu chache kwenye Ligi Kuu ambayo kila msimu inakuja na asilimia kubwa ya wachezaji wale wale. Huwa inabadilisha makipa tu. Lakini ukiangalia wachezaji wengi wa timu hiyo wameichezea klabu hiyo zaidi ya miaka 10, kitu ambacho kinaonyesha kulihitajika marekebisho makubwa kwenye kikosi.

Baadhi tayari umri umeshaanza kuwatupa mkono, hawana mguvu, kasi kama ile ya mwanzo, hivyo walihitaji wachezaji wengine wa kuwasaidia. Nashangaa tangu mzunguko wa kwanza Prisons haikuwa inafanya vizuri, lakini haikulitumia dirisha dogo kufanya usajili wa maana kama wenzao Geita Gold walivyofanya.

Ni kweli Prisons haiwezi kuwaondoa wachezaji wake kirahisi kwa sababu asilimia kubwa ni askari, lakini walihitaji msaada kutoka kwa wachezaji wengine.

Wachezaji kama Salum Kimenya, Samson Mbangula, Jeremiah Juma, Benjamin Asukile, Jumanne El Fadhili, na wengineo, ni wa muda mrefu kwenye kikosi hicho na wamekuwa wakicheza misimu yote mfululizo, wakiwa kwenye kikosi cha kwanza, hivyo ni lazima watakuwa wamechoka, wanahitaji kupumzika na kucheza mara chache.

Kwa bahati mbaya sana ni kwamba Prisons imechelewa, viongozi hawakusoma alama za nyakati. Kinachotakiwa sasa ni kupambana, kama ikifanikiwa kubaki Ligi Kuu, kuna kazi kubwa ya kufanya msimu ujao kwa kusajili damu changa na hao wakongwe wawe wanawasaidia na si wote kucheza.

Haitakuwa vizuri kupoteza timu kama Prisons kwenye Ligi Kuu, timu iliyolitendea haki soka la Tanzania kwa kuzalisha wachezaji kama kina Primus Kasonso, Henry Morris na wengine wengi walioibukia hapo kuwa wachezaji wakubwa nchini.

# ‘Saratani shingo ya kizazi tishio kwa wanawake’

**Na Beatrice Shayo**

RAIS wa Chama cha Madaktari Bingwa ya Wanawake na Watoto (AGOTA), Dk. Matida Ngarina, amesema kuna changamoto ya baadhi ya wagonjwa wenye saratani kukwepa kupigwa mionzi na kutafuta njia mbadala ya miti shamba hali inayo hatarisha usalama wa afya zao.

Ngarina ambaye ni Daktari Bingwa wa magonjwa ya wanawake katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akitoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wanaweka kuhusiana na umuhimu wa kufanya vipimo mapema kwenye saratani ya shingo ya kizazi na matiti yaliyoandaliwa na Hospitali ya Massana.

Alisema kutokana na kukosa uelewa wengine wakisikia mionzi wanaona kama jua litawachoma usoni na kubabuka jambo ambalo sio la kweli.

“Kuna hili jambo la watu kuogopa mionzi pale mgonjwa anapojulishwa katika matibabu anatafuta njia mbadala ambayo kwake anaona anayeweza kuimudu kuliko hii ambayo namwambia hii ndiyo shida ambayo tunaipata,” alisema.

Alisema mgonjwa anatumia mitishamba badala ya mionzi na anapozidiwa akifikishwa hospitali yupo hatua mbaya kutokana na kukaidi maagizo aliyopewa.

Alisema tatizo jingine walokutana nalo wanavyotibu wagonjwa wa saratani ya shingo wa kizazi watu wengi hawana uelewa kwa sababu ugonjwa wenyewe umekaa sehemu ya mafichoni watu wanachelewa kufika katika vituo vya afya.

“Tunapata wagonjwa ambao wamefikia hatua mbaya ya ugonjwa hatua ambayo naweza kumsaidia mgonjwa ni kupata mionzi, watu hawana uelewa wa kufanya uchunguzi mapema kama inavyotakiwa huu ugonjwa ungepungua na kuondoka,” alisema.

Dk. Ngarina alisema kama Watanzania wangezingatia kufanya uchunguzi mapema ingesaidia mtu kujua hatua za awali kabla ya kubadilika kufikia saratani kwa kuwa ugonjwa huo unatibika mtu anapouwahi.

Alisema kwa Hospitali ya MNH nusu ya kinamama waliolazwa katika wodi ya wenye magonjwa ya saratani ya shingo ya kizazi na Ocean Road wana saratani ya shingo ya kizazi.

“Ni saratani ya shingo ya kizazi inayoongoza hivyo kuna haja ya kutoa elimu kwa wingi ili wajitokeze katika kufanya vipimo mapema badala ya kuchelewa unakuja kuambiwa upo ugonjwa katika hatua mbaya ambayo huwezi kupona,” alisisitiza.

Naye Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Saratani kutoka Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Dk. Nanzoke Mvungi, alisema saratani ya shingo ya kizazi na matiti ni magonjwa yanayowasumbua wanawake na kushauri watoto wa kike kuacha kushiriki ngono isiyo salama katika umri mdogo ili kujikinga na maradhi hayo.

Alisema watoto wa kike wanaoanzia miaka tisa kabla hawajaanza kushiriki katika matendo ya ngono wanatakiwa kupata chanjo, kwa kuwa kirusi kinachoeneza saratani ya shingo ya kizazi kinaweza kudhibitiwa na chanjo inayotolewa na Ocean Road.

Alisema wanawake katika kujikinga na mgonjwa hayo wanashauriwa kufanya uchunguzi wa awali wa saratani ili kujikinga na ugonjwa huo.

Naye Mkurugenzi wa Tiba Hospitali ya Massana, Dk. Robert Josiah, alisema wametoa elimu hiyo baada ya kubaini kuwapo kwa wanawake wengi wanaosumbuliwa na saratani hiyo huku wengi wao wakishindwa kupata tiba kwa kukosa elimu sahihi.

Alisema wanawake wanatakiwa kwenda vituo vya afya mara kwa mara kufanya uchunguzi wa afya ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kujitibu mapema na tatizo kuisha.

# Malengo matatu kurahisisha upatikanaji maji vijijini haya

**Na Maulid Mmbaga**

MKURUGENZI Mkuu wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mhandisi Clement Kivegalo, amebainisha malengo matatu yanayolenga kurahisisha upatikanaji wa maji vijijini ikiwamo kuanzisha mfumo mpya wa kusanifu miradi kwa kutumia vyanzo vikubwa vya maji.

Aliyasema hayo juzi mkoani Dar es Salaam katika mjadala maalumu wa kuonyesha mafanikio ya mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan uliokuwa ukifanyika Azam TV, alisema watatumia vyanzo vikubwa kama maziwa kuhudumia vijiji vingi kwa wakati mmoja.

Pili alisema ni kupunguza gharama za maji vijijini ili yawe yapatikane kwa urahisi na watatu ni kuanzisha mfumo wa malipo kabla ya huduma na wanatarajia mwezi ujao kuingia makubaliano ya kimkataba na Chuo cha ufundi cha Arusha, Dar es Salaam na Mbeya ambao wameshawahakikishia kwamba wana uwezo wa kuandaa mifumo husika ambayo itatumika kirahisi na watu wa kijijini.

“Tunataka tuunganishe na mifumo ya simu za mikononi ili mimi nikiwa huku mjini naweza nikamnunulia maji mama yangu kijijini nikalipa akaenda kuchota maji kwa kutumia kadi, hayo ndiyo maeneo ambayo tunataka kuyapa kipaumbele ili kupunguza gharama lakini na kurahisisha upatikanaji wa maji vijijini,” alisema Kivegalo.

Pia alisema katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia wamepata mafanikio mbalimbali ikiwamo kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji vijijini pamoja na kutekeleza miradi 522 na kupeleka maji kwenye vijiji vipya 1,560 ambavyo vimewezesha zaidi ya watu milioni mbili kupata huduma hiyo.

Alibainisha kuwa wakati Rais Samia anaingia madarakani kiwango cha upatikanaji wa maji kilikuwa ni asilimia 72.3 na sasa ni 74.2 akisisitiza kuwa ongezeko hilo ndani ya mwaka mmoja kwenye sekta ya maji ni kubwa.

Aliongeza kuwa kuundwa kwa RUWASA kumesaidia kudhibiti huduma ya maji vijijini na alibainisha kuwa wameshaanza kuandaa miongozo na mafunzo ili kuhakikisha huduma hiyo inatolewa kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo ya serikali.

Aidha, alikiri kuwa wakati wa kiangazi maji yakipungua hata uzalishaji nao unashuka na kupitia ujenzi wa bwawa la Kidunda asilimia kubwa ya maji yatabaki huko ambapo wakati wa kiangazi yataachiwa ili kuwezesha mitambo kufanya kazi muda wote.

Alisema Rais ameipatia RUWASA Sh. bilioni 79.5 ambapo wanatarajia kutekeleza miradi mingine kwenye vijiji 331 na kupitia vijiji hivyo wananchi zaidi ya milioni 1.36 watapata huduma ya maji, na kupitia fedha za UVIKO-19 wanatarajia kununua seti 25 za mitambo ya uchimbaji wa visima.

“Rais amedhamiria kumtua mama ndoo kichwani, lakini kuna fedha zimetengwa kununua seti tano za mitambo ya ujenzi wa mabwawa, pia kuna seti nne za vifaa vya kutafiti maji chini ya ardhi na Wizara ya Maji tayari imeshasaini mikataba na wauzaji wa mitambo hiyo,” alisema Kivegalo.


TPA TANZANIA PORTS AUTHORITY

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA

Salaam za Pongezi

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa **Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)** Tunakupongeza kwa utendaji na uwajibikaji wako katika kusimamia na kutekeleza yale uliyoyaahidi ndani ya kipindi hiki cha mwaka mmoja.

*Tunakuombea afya njema na tuko pamoja katika kuhakikisha agenda ya maendeleo ya Watanzania inafanikiwa.*



MH. SAMIA SULUHU HASSAN
RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# HABARI KITAIFA



Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis, akipata maelezo kutoka kwa msimamizi wa mauzo wa Kampuni ya Nestle Co.Ltd, Prisca Biseko, namna ya kutengeneza maziwa ya watoto kwenye maonyesho ya mwanamke kinara yaliyoandaliwa na EATV, mkoani Dar es Salaam.



Watangazaji wa kipindi cha Dadaz kinachorushwa na EATV wakielezea utaratibu ulivyo wa watoto kwenye sherehe za Mwanamke Kinara iliyoandaliwa na EATV, jana.




Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis (kushoto), akiwa pamoja na Mkurugenzi wa EATV, Regina Mengi (wapili kushoto), kwenye sherehe za Mwanamke Kinara, jana mkoani Dar es Salaam.




Washiriki wakimsikiliza Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis (hayupo pichani), kwenye sherehe za Mwanamke Kinara.



Naibu Waziri, Mwanaidi Ali Khamis, akiongea na washiriki kwenye sherehe za Mwanamke Kinara jana, mkoani Dar es Salaam.




Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis (wapili kulia), akiendesha kongamano la biashara, kwenye sherehe za Mwanamke Kinara. Kulia ni Msaidizi wa Usajili (Wakala wa Biashara na Leseni Brela), Maryglory Mmary, Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa United Bank for Afrika, Brendansia Kileo (kushoto), na Mkurugenzi wa Biashara Tanzania Distilleries Ltd (TDL, Temea Chogo.




Washiriki wa hafla ya Mwanamke Kinara wakiburudishwa na muziki kutoka kwa msanii Mwasiti Almas, jana. Katikati ni Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe.



Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis, akipokea cheti kwa Mkurugenzi Mtendaji wa EATV, Regina Mengi, cha kutambua mchango wa Rais Samia Suluhu Hassan, kwenye sherehe za Mwanamke Kinara. **PICHA ZOTE: MIRAJI MSALA**

# Tigo, Samsung zaja na Samsung S22

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Tigo Tanzania, imeshirikiana na Samsung Electronics kuzindua simu janja za Samsung S22 Tanzania.

Ushirikiano huo ni sehemu ya harakati za kampuni hiyo ya mawasiliano kuongeza matumizi ya mtandao wa teknolojia ya 4G nchini.

Mkuu wa Kitengo cha Maduka na bidhaa za intaneti, Mkumbo Myonga, akizungumza wakati wa uzinduzi huo wa simu za kisasa za Samsung S22, alisema:

"Tigo inashirikiana tena na Samsung Tanzania kuweka na kuuza simu za kisasa za Samsung S22. Utatu wa simu hizo ni pamoja na Galaxy S22, S22+, S22 Ultra. Hii inaonyesha shauku yetu ya kubadilisha anga ya kidijitali ya Tanzania kwa kutumia simu mahiri ya hali ya juu, ambayo itafanya matumizi ya intaneti ya mteja iwe ya kufurahisha zaidi."

"Pamoja na maendeleo yaliyopatikana katika kuboresha utumiaji wa simu za kisasa, bado kuna nafasi ya kuboreshwa na ndiyo maana, tunaendelea kuwekeza katika ubia unaolenga kutoa matokeo yanayotarajiwa ya kupita kwa karibu asilimia 100 katika siku za usoni." aliongeza Myonga.

Myonga alifafanua zaidi kuwa: "Wateja watafurahia matumizi bora ya kidijitali kupitia mtandao wetu wa kasi zaidi wa 4G ambao ni mkubwa zaidi nchini. Baada ya kununua Samsung S22 tunatoa data ya intaneti ya GB 96 BILA MALIPO kwa mwaka mzima kwa wateja wote wanaonunua simu mahiri za mfululizo wa Samsung S22."

Meneja Mkazi wa Kampuni ya Samsung Tanzania, Suleiman Mohamed, alisema

"Samsung Electronics leo imezindua Galaxy S22 Ultra, ikiunganisha sifa bora zaidi kati ya mbili za simu za kisasa – uwezo usio na kifani wa mfululizo wa note na kamera ya daraja la juu na utendakazi wa mfululizo wa S – kuweka kiwango kipya cha simu mahiri za ubora.

# TBA yashauriwa kutatua mgogoro nyumba Wazo

**Na Maulid Mmbaga**

MWENYEKITI wa Serikali ya Mtaa wa Wazo Halmashauri ya Kinondoni, Dar es Salaam, Medard Mashauri, ameushauri Wakala wa Nyumba Tanzania (TBA) kufuatilia na kutatua mgogoro unaoendelea katika eneo hilo kuhusu mmoja wa wakazi wake kutolewa katika makazi yake kinyume cha taratibu.

Katika Mtaa wa Wazo kuna nyumba ambazo zinasimamiwa na TBA ambazo zimepangishwa kwa wananchi na inadaiwa kuwa Februari 2021 Elieka Nyiti alitolewa katika makazi yake na kupatiwa mtu mwingine kwa madai kuwa alishindwa kulipa deni la kodi ya pango Sh. milioni 8, hivyo kuwa chanzo cha mgogoro unaoendelea.

Akizungumza wakati wa kikao kilichomhusisha yeye, wawakilishi kutoka TBA na wananchi, alishauri wenye mamlaka kuwa watazame jambo hilo kwa sura nzuri na kama nyumba husika itakuwa inasoma jina mkazi huyo huyo basi wamrudishie. Pia aliwashauri wananchi kuwa wawape nafasi TBA wakakae na kulizungumza suala hilo kwa kuwa sio jambo la mtu mmoja, huku akisema kuwa endapo hawatatoa mrejesho kwa wakati, basi watachukua hatua za kufuata utaratibu mwingine.

"Tushirikiane mkiona TBA wameingia bila kupitia katika ofisi ya serikali ya mtaa niambieni kwa sababu hata polisi wanapokuja kumwondoa mtu lazima waje hapa, kama watakuja kinyemela tushirikishane mimi nitampigia ninayetakiwa kumpigia halafu atusaidia kuwa hawa watu wametumwa na nani," alisema Mashauri.

Kwa upande wake, mlalamikaji alidai kuwa alitolewa katika makazi yake kimabavu na bila mamlaka hiyo kutoa taarifa ya utekelezaji wa suala hilo kwa uongozi wa mtaa huo, na kwamba yuko tayari kupokea maamuzi yoyote yatakayoamuliwa na

TBA, huku akidai kuwa amesumbuka kwa muda mrefu kutafuta haki yake bila mafanikio.

"Mwende mkalijadili mkiamua nyumba nipewe sawa, mkiamua kuwa sifai sawa hakuna kitu Gilbert asichokijua... nimeenda mara nyingi kufuatilia hili suala wameninyanyasa sana, mimi siendi tena huko, tangu lini mnyonge akashinda na wewe ndio mkubwa," alisema Elieka.

Mwakilishi kutoka TBA, Gilbert Mwasambo, ambaye anashughulikia mgogoro huo, alisema wataenda kukaa kikao na yale ambayo watakubaliana wakati wa kutoa maamuzi juu ya suala hilo watamuita mwenyekiti ili waweze kuongea na mama huyo.

Aidha, aliwaeleza wananchi hao kuwa kama wanaona wamekosewa wanapaswa kwenda kwa mwenyekiti au kwenye mamlaka husika, huku akisema kuwa wakazi wa eneo hilo hawana mamlaka yoyote ya kufanya mabadiliko katika nyumba hizo, kutokana na shinikizo lao wakitaka aliyekabidhiwa nyumba hiyo atolewe.

"Nyinyi hamna mamlaka yoyote ya kufanya mabadiliko pale mpaka mje TBA na hao ndio wawasiliane na mwenyekiti kwa sababu ndiye yuko karibu na watu, suala la mtu kukaa kwenye nyumba ni la TBA na uongozi ulioko," alisema Mwasambo.

"Tulimwandikia barua ya kumkumbusha kuhusu deni lake na hakujibu kwa hiyo sisi nyumba tulikuta imefungwa, kabla ya kumweka yule tuliifunga maana yake tulikuwa tunataka kama kuna mtu mwenye mali au anaishi pale atakuja atapiga simu kwamba nyumba yangu imefungiwa halafu sisi tutajua jinsi ya kufanya," alisema Mwasambo.



Mkuu wa Kitengo cha Biashara-GetPaid, Justine Mahinyila, akifafanua jambo kwa waandishi wa habari, wakati wa uzinduzi rasmi wa Jukwaa la GetPaid, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA NA MPIGA PICHA WETU**

# Jukwaa la 'GeitPaid' kuwapa fursa Watanzania

**Na Mwandishi Wetu**

JUKWAA la Kijiditali, 'GetPaid' lenye lengo la kutoa fursa za ajira na nyinginezo limezinduliwa jijini Dar es Salaam, ikiwa ni sehemu ya mchango wa sekta binafsi kusaidia mikakati ya serikali inayolenga kupanua wigo wa fursa kwa vijana na Watanzania kwa ujumla.

Mbali na mambo megine Jukwaa la GetPaid, litasaidia Tanzania kupunguza wimbi kubwa la ukosefu wa ajira kwa vijana na Watanzania wote (wasomi na wasiosoma), alisema Richard Lema, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Tanzania DLT CP iliyobuni na kutengeneza Mtandao wa GetPaid wakati wa uzinduzi rasmi wa Jukwaa hilo jijini Dar es Salaam jana.

Kwa mujibu wa Lema, GetPaid ni jukwaa la kimkakati la kidijitali ambalo lengo lake kuu ni kuwaunganisha Watanzania, likiwa na nia ya pamoja na vijana, wafanyabiashara, wasomi, wasiosoma, wajasiriamali, wanaofanyakazi binafsi na fursa mbalimbali duniani.

Alielezea GetPaid kama ni teknolojia ya kisasa, ambayo itawaunganisha watu na fursa mbalimbali kitaifa, kikanda na kidunia.

Kwa njia ya Jukwaa la GetPaid, watu wa aina mbalimbali wazalishaji, wafanyabiashara, wanaofanya kazi binafsi, watu wazima, vijana, wenye weledi watawezeshwa kunufaika na fursa mbalimbali zilizoko Afrika na nje ya Afrika.

"Jukwaa la GetPaid linawafanya waweze kunufaika na fursa mbalimbali duniani, elimu ya kidijitali na uvumbuzi. Hili linafanyika kupitia kikundi cha jumuiya, utumiaji rahisi na elimu," alisema Lema na kuongeza kwamba "bidhaa ya GetPaid ina vitu vitatu na inawapa watumiaji (waanzilishi, wafanyabiashara na wafanyakazi binafsi vifaa na elimu wanayohitaji kuishi, kufanyakazi na kupata ujira."

Akizungumza wakati wa uzinduzi, Mtaalamu wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari (ICT), Baraka Mafore, alisema ingawa kuna ukuaji wa kasi wa uchumi wa kidijitali, bado kuna pengo kubwa linalotakiwa lijazwe, kwa vile mamilioni ya vijana katika nchi nyingi za Afrika hawana ajira.

Takwimu za hivi karibuni zinaonyesha pamoja na kwamba vijana wanaomaliza chuo na kuingia kwenye soko la kazi Tanzania wanaanzia 800,000 hadi 1,000,000 kila mwaka (NBS-2015), kwa wastani uchumi unatengeneza ajira zipatazo 250,000 tu kwa mwaka na asilimia 75 ya vijana hawa wanabaki bila ajira.

"Hata hivyo, kutumia njia na vifaa sahihi, kama Jukwaa la GetPid, nchi za Afrika zinaweza kushuhudia idadi kubwa ya vijana wakijiunga na kuingia kwenye uchumi wa kidijitali," alisema mhitimu mmoja kutoka Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam (UDSM), Asha Mkwezu wakati wa uzinduzi wa GetPaid APP.

# RC Gabriel afunguka upandaji wa miti

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WANANCHI wametakiwa kutambua umuhimu wa upandaji miti na utunzaji kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa bidhaa na huduma za misitu nchini.

Rai hiyo ilitolewa jana jijini Mwanza na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya maadhimisho ya siku ya upandaji miti na Siku ya Misitu Duniani.

Gabriel alisema maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani yanatokana na azimio la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa la mwaka 2012 ambalo liliagiza nchi wanachama kuadhimisha siku hiyo kila ifikapo Machi 21 ya kila mwaka.

"WanaMwanza na Watanzania wote kwa ujumla mnatakiwa kuhakikisha suala la upandaji miti kila kaya linakuwa endelevu na utunzaji na uhifadhi wa misitu kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo," alisema Gabriel.

Alisema juhudi za upandaji miti katika mkoa wa Mwanza zilianza kwa kampeni kabambe iliyozinduliwa Desemba 9 mwaka 2021 katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza na kilele chake kilikuwa Februari 26 mwaka huu katika Manispaa ya Ilemela.

"Katika kipindi cha mwaka 2021 na 2022 tumefanikiwa kupanda miti 3,237,871 kati ya hiyo iliyostawi ni 2,816,948 sawa na asilimia 87 na miti 420,923 sawa na asilimia 13 ilinyauka na kuharibika," alisema Gabriel.

Aidha, Gabriel alisema licha ya kuwapo juhudi za kutunza misitu, bado kuna vikwazo katika sekta hiyo ikiwamo ukame, mifugo, wadudu waharibifu, magonjwa na elimu ndogo ya umuhimu wa misitu kwa wananchi.




Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya NMB, Juma Kimori, akiwasilisha salamu za NMB kwenye kongamano la tathmini ya mwaka moja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan lililofanyika katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), jijini Dodoma, ambalo lilishirikisha wataalamu kutoka ndani na nje ya nchi pamoja na wanafunzi. NMB ilikuwa mdhamini mkuu wa kongamano hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miti 3,800 kwenye Mto Nyakasangwe

**Na Frank Monyo**

BODI ya Bonde la Wami/Ruvu ofisi za Dar es Salaam, katika kuelekea kilele cha Wiki ya Maji imepanda miti 3,800 kwenye kingo za Mto Nyakasangwe uliopo eneo la Dovya Kata ya Bunju, Dar es Salaam ili kunusuru nyumba zaidi ya 50 kusombwa na maji zilizoko pembezoni mwa mto huo.

Akizungumza na wananchi wa eneo hilo wakati wa kupanda miti hiyo juzi, Meya wa Kinondoni, Songoro Mnyonge, alisema Manispaa ya Kinondoni imeungana na Bonde la Wami/Ruvu kuadhimisha Wiki ya Maji ambayo imeanza Machi 16, 2022 ambapo kitaifa yatahitimishwa Machi 22. Alisema anatambua kuwa mto huo unapitisha maji mengi na umeleta athari kwa wakazi wa Kinondoni na wilaya za jirani ambazo zinapitiwa na mto huo wakati wa vipindi vya mvua.

"Kwa hapa ambapo tupo Kata ya Bunju Mtaa wa Dovya, zaidi ya nyumba 60 ambazo zilikuwa kwenye maeneo halali kabisa zilisombwa na maji ya mto huu na kufanya wananchi hao kuwa masikini. Kwa kutambua hilo wenzetu wa bonde wameona ni lazima tulinde mazingira kwa kudhibiti mmomonyoko wa mto huu kwa kupanda miti," alisema Mnyonge.

Alisema zoezi la kupanda miti hiyo linafanyika baada ya mto huo kusafishwa kwa ushirikiano wa Bonde la Wami/Ruvu, Manispaa ya Kinondoni pamoja na Baraza Taifa la Hifadhi na Usimamizi la Mazingira (NEMC) na kupunguza makali ya mto huo kwa kutengeneza njia nyingine ya maji kupita na kuacha kupita kwenye makazi.

"Mvua zilizonyesha hivi karibuni zimetuonyesha majibu, baada ya maji katika mto huu kutembea vizuri hayakuleta athari, lakini pamoja na hilo tukaona ni lazima tudhibiti mmomonyoko, leo tumekuja hapa kupanda miti 3,800 ila kwa kuanzia tutaanza na miti 300 kutokana na hali ya hewa lakini hapo baadaye mvua zitakapoanza miti yote itapandwa," alisema.

Halima Faraji, Ofisa Bonde la Wami/Ruvu ofisi ya Dar es Salaam, alisema sehemu ilipopandwa miti hiyo ni sehemu korofi kwani mto uliacha njia yake na kuathiri makazi ya watu kwa kiasi kikubwa.

"Sisi kama Bonde la Wami/Ruvu wenye dhamana ya kusimamia mito kisheria kwa mujibu wa sheria za rasilimali za maji, Sheria No.11 ya 2009, kwa hiyo tumekuja hapa kushiriki na wananchi pamoja na serikali za mitaa pamoja na kamati ya kuratibu shughuli za usafishaji wa mito ya mkoa wa Dar es Salaam yenye lengo la kusimamia maisha ya watu na makazi yake yanakuwa salama," alisema Halima.

Alisema kuwa Bonde la Wami/Ruvu katika kusherehekea Wiki ya Maji inaungana na Rais Samia Suluhu Hassan kwenye kusimamia rasilimali za maji ili kuhakikisha uhakika wa upatikanaji wa maji pamoja na kuhakikisha mama anatua ndoo kichwani.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Dovya Kata ya Bunju Wilaya ya Kinondoni, Razalous Mwakiposa, alilishukuru Bonde la Wami/Ruvu kwa kupanda miti kwani wananchi wa eneo hilo walikuwa wanateseka pindi mvua zinaponyesha. "Kabla ya zoezi la kutengeneza mto huo kwa kuusafisha nyumba zaidi ya 60 zilisombwa na maji watu wamehama makazi yao watu wameingia hasara, lakini maamuzi ya kamati iliyoundwa kwa ajili ya mto huu tulishauriana tuupasue mto na kuunyoosha baada ya kuchora S, na hili la kunyoosha limeleta manufaa makubwa kwani mvua zilizonyesha hivi karibuni wananchi wa eneo hilo wamepona hakuna madhara yoyote yalitokea," alisema Mwakiposa.

# Balozi wa Tanzania nchini Marekani alivyokaribishwa

**Na Mwandishi Wetu**

BALOZI mpya wa Tanzania nchini Marekani, Elsie Kanza, amepata mapokezi makubwa nchini humo.

Balozi Kanza alikaribishwa kwenye mji mkuu Washington DC na viongozi wa Marekani walioko kwenye mji huo.

Sherehe hiyo iliandaliwa rasmi na kampuni ya Pula Group inayomilikiwa na Balozi wa Marekani mstaafu nchini Tanzania, Charles Smith na Dk. Mary Smith kwenye ofisi za wanasheria za Capitol Hill, Nelson Mullins.

Miongoni wa viongozi mbalimbali kutoka serikalini na sekta binafsi walihudhuria ni Naibu Waziri wa Biashara, Don Graves, Mkurugenzi Mkuu wa Corporate Council on Africa Florie Liser, Mkurugenzi Mkuu wa Constuency for Africa Mel Foote. Pia walikuwapo wabunge wa Congress Al Green na Emmanuel Cleaver.

Akizungumza Rais wa Pula Group, Mary alisema, "lengo letu tunataka kumfanya Balozi Kanza awe kiongozi bora mwenye maamuzi sahihi ndani ya ofisi hizi hapa Washington." "Hiyo itafanya kuwawezesha Watanzania kupata fursa nyingi," alisema Balozi Charles Smith ambaye ni mwenyeki wa Pula Group.

Aliongeza: "Tunaamini Tanzania ni sehemu sahihi kufanya biashara na uwekezaji kwa sababu ya uongozi bora". Tunaona uongozi wa Rais Samia Hassan na baraza lake ulivyo makini katika utekelezaji."

Nipashe
Spotika




WACHEZAJI WA5 WALIOKO KWENYE KLABU ISIYO SAHIHI UK. 12-13



RONALDO

SON

# NYOTA WATANO WENYE HAT-TRICK NYINGI DUNIANI

**LONDON,** England

KUFUNGA mabao matatu 'hat-trick' katika mechi moja ya mpira wa miguu ni ndoto ya kila mwanasoka. Baada ya yote, kufunga mabao ndio lengo kuu la timu yoyote na kuchangia kwa sababu ni dhamira ya kila mchezaji anayehusika.

Kila bao lililofungwa katika mchezo ni muhimu. Kwa mchezaji kuwa mtawala sana hivi kwamba anatikisa wavu mara tatu katika mchezo mmoja ni mafanikio makubwa. Tumeona wafungaji mabao wengi wakishinda ulimwengu katika miongo kadhaa iliyopita.

Katika karne ya 21, tumeona washambuliaji wakiinua kiwango cha juu na kufikia viwango vya tija ambavyo bado tunavizoea. Bila kuchelewa, tuangalie wachezaji watano waliofunga hat-trick nyingi zaidi katika historia ya mchezo huo, haya sasa...

**#5. LUIS SUAREZ - HAT-TRICK 29**

Luis Suarez ni mmoja wa washambuliaji wakubwa wa zama za kisasa. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay alikuwa mzuri wakati wa miaka yake ambayo alikaa Liverpool na Barcelona.

Suarez alihamia Barcelona mwaka 2014 na kuunda utatu wa wachezaji watatu Lionel Messi na Neymar.

Kati ya misimu ya 2009-10 na 2018-19, ni mchezaji mmoja tu aliyewashinda Cristiano Ronaldo na Lionel Messi kwa kutwaa Kiatu cha Dhahabu cha Ulaya kwa ufungaji bora kwa ligi kubwa tano. Mchezaji huyo ni Luis Suarez. Alishiriki na Cristiano Ronaldo msimu wa 2014-15 kabla ya kushinda moja kwa moja msimu wa 2015-16.

Suarez amefunga hat-trick 29 katika maisha yake ya soka, sawa na Robert Lewandowski.

**#4. ROBERT LEWANDOWSKI - HAT-TRICK 29**

Mchezaji huyo wa Bayern Munich ndiye mshambuliaji mahiri zaidi duniani kwa sasa. Lewandowski amekuwa akivunja rekodi za kufunga mabao kwa kujifurahisha zaidi ya miaka michache iliyopita.

Katika msimu wa 2020-21, alivunja rekodi ya Gerd Muller ya kufunga mabao mengi zaidi katika msimu mmoja wa Bundesliga (40) kwa kufumania nyavu mara 41 katika mechi 29.

**#3. LIONEL MESSI - HAT-TRICK 55**

Lionel Messi ni mmoja wa wafungaji bora wa wakati wote. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina pia bila shaka ndiye mwanasoka bora zaidi wa wakati wote. Ameshinda Ballon d'Or, tuzo ya binafsi yenye hadhi zaidi katika soka, akiweka rekodi kwa kuibeba mara saba.

Messi ni mmoja wa washambuliaji waliokamilika na amefunga hat-trick 55 katika maisha yake yote.

Messi amekuwa na msimu mgumu katika suala la mabao kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1 msimu huu. Hiyo ndiyo aina mbaya zaidi ya ufungaji kuwahi kuonyeshwa katika maisha yake ya soka.

**#2. CRISTIANO RONALDO - HAT-TRICK 59**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37, alirudi nyuma miaka iliyopita na kutoa kiwango cha hali ya juu na kufunga hat-trick yake ya 59 katika maisha yake ya soka na kushinda mchezo kwa United. Ronaldo, kama ilivyo kwa FIFA, ndiye mchezaji aliyefunga mabao mengi zaidi kwa klabu na nchi akiwa na mabao 806.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno alifunga hat-trick 59.

**#1. PELE - HAT-TRICK 92**


Uhalisi wa vyanzo vinavyounga mkono madai ya upachikaji mabao wa Pele bado unashukiwa kusema kidogo. Lakini hatuwezi kupuuza ukweli kwamba gwiji huyo wa Brazil ni mmoja wa wachezaji bora kuwahi kupamba mchezo huo. Orodha yake ya ajabu ya mafanikio inathibitisha ukweli huo.

Pele ameripotiwa kufunga hat-trick 92 kwa klabu na nchi katika maisha yake ya soka. Inasemekana kuwa hat-trick zake nyingi kati ya 92 zilikuja katika michezo ya kirafiki na hakuna njia ya kuthibitisha ni ngapi kati ya hizo zilichukuliwa kuwa rasmi.

Lakini Kitabu cha Rekodi za Dunia cha Guinness kinamtambua Pele kuwa ndiye mchezaji aliyefunga hat-trick nyingi zaidi katika historia ya soka akiwa na mabao 92. Pia anashikilia sifa ya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kufunga hat-trick kwenye Kombe la Dunia. Pele alifungia Brazil mwaka 1958 akiwa na umri wa miaka 17. Rekodi hiyo bado haijavunjwa kwa miaka 64 sasa.

## ISIKUPITE

MABAO mawili aliyofunga Robert Lewandowski juzi, Jumamosi wakati Bayern Munich ikishinda 4-1 dhidi ya Union Berlin, yanamfanya kucheka na nyavu mara 31 hadi sasa kwenye Bundesliga msimu huu. Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Poland sasa amefunga mabao 30 ama zaidi kwa misimu mitano, akiifikia rekodi iliyowekwa na nguli wa Ujerumani, Gerd Muller, lakini kwa msimu huu amefikisha mabao 43 katika mashindano yote kwa Bayern.



# WACHEZAJI WA5 WALIOKO KWENYE KLABU ISIYO SAHIHI



POGBA

**LONDON,** England

KILA madirisha ya uhamisho ya wachezaji huleta mzunguko mwingine wa hatua za kuvutia na mikataba ya kushangaza. Timu kubwa barani Ulaya huchagua wachezaji wanaowapenda kutoka kwa timu ndogo; wakati mwingine mchezaji atabadilisha upande wake mkubwa kwa mpinzani.

**Ingawa baadhi ya uhamisho mkubwa wa siku za hivi karibuni umekuwa wa mafanikio makubwa - fikiria Cristiano Ronaldo kwenda Real Madrid kutoka Manchester United, Juventus na baadaye kurudi tena Old Trafford.**

Hii inaweza kuwa ni suala la mtindo, au inaweza kuwa kutokana na ushindani mkali wa nafasi katika kikosi.

Makala haya yanaorodhesha mifano mitano ya sasa ya wachezaji ambao wako kwenye klabu ambazo si sahihi kwao kuzichezea, twende sasa...

### #5. PAUL POGBA (MANCHESTER UNITED)

Pogba amekuwa na kampeni ya kupanda na kushuka pale Manchester hadi sasa.

Wakati wa zama za kocha Jose Mourinho, alipendelea zaidi kumtumia Scott McTominay asiye na uzoefu kuliko Mfaransa huyo, na hiyo ikafanya hali kuwa mbaya kwa mchezaji ambaye aliwahi kushikilia rekodi ya kununuliwa kwa ada ya juu zaidi duniani.

Alipokuwa Juventus kabla ya kurejea Manchester United, alicheza katika safu ya kati ya wachezaji watatu, ambayo ilimruhusu kuwa mchezaji mzuri.

Tofauti iliyoko sasa ni kwamba anaombwa kufanya mambo mengi sana; umuhimu wa Pogba kwa timu yake ni mkubwa, lakini yeye si mchezaji wa aina hiyo.

Alikuja katika timu ya Man United katika kipindi cha mpito ingawa ingekuwa bora kama angebaki Juventus, ambapo aliabudiwa na timu ingejengwa kupitia yeye.

Kuhamia Real Madrid kungekuwa na maana pia, kwani klabu hiyo kwa sasa iko mbele ya Manchester United kwa mafanikio.

### #4. ISCO (REAL MADRID)

Kuna wachezaji wachache wanaopendeza zaidi katika soka la dunia wanapokuwa katika kiwango cha juu. Msimu wa 2016-2017 ulionekana kuwa mwaka wa mapumziko kwa kiungo huyo wa kati katika klabu ya Real Madrid, kwani alikuwa na nafasi kubwa kutokana na kutokuwapo kwa Gareth Bale.

Ilikuwa ni ujanja wake na uchezaji mpira katikati ya uwanja ambao uliruhusu timu yake kuipiku Barcelona kwenye taji la Ligi Kuu.

Takwimu za Isco kwa kampeni hiyo ni nzuri, lakini amejikuta akiingia na kutoka nje ya timu, akijitahidi kupata uthabiti.

Alikuwa na mchango katika mabao 10 kwenye La Liga katika mechi 18 pekee, lakini kocha Zinedine Zidane alipendelea kuwatumia zaidi Luka Modrićna Toni Kroos kuliko Mhispania huyo.

Ni kweli kwamba, Real Madrid wamejazwa vema katika safu ya kiungo, hata Marco Asensio alisimamia mechi 14 tu kwenye ligi, lakini Isco hakika anastahili kuwa katika kikosi cha kwanza mara kwa mara.

Anaonekana kama ndiye anayefaa kuchukua mikoba ya Andres Iniesta baada ya kustaafu pale Hispania.

Klabu za Uingereza zilipaswa kupanga foleni kumsajili na, ikizingatiwa anacheza sawa na David Silva, si vigumu kufikiria kuwa angekuwa na mafanikio kwenye Ligi Kuu England.

Staili yake ya uchezaji ingemfaa zaidi pale Arsenal, bila shaka, na mchezaji huyo anaweza tu kufurahia nafasi ya kuwa mtu mkuu katika klabu, jambo ambalo halitawezekana akiwa Real Madrid pamoja na nyota wao wote.

### #3. NEYMAR (PSG)

Inaweza kuonekana kuwashtua wengi kumjumuisha mchezaji ghali zaidi duniani kwenye orodha hii, haswa ikizingatiwa jinsi alivyofanya vizuri tangu ajiunge na PSG, lakini kuna idadi kubwa ya watu wanaofikiria kuwa Mbrazil huyo Ufaransa si sehemu sahihi kwake.

Lengo lilikuwa kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini msimu huu tayari wametolewa mapema na Real Madrid hatua ya 16-bora, na hamu ya kushinda taji hilo ndio sababu kuu iliyomfanya ajiunge na klabu hiyo.

Ligi mara zote ilielekea kuwa ya PSG na hii imeendelea kuwa hivyo, lakini changamoto nchini Ufaransa haitoshi kwa mchezaji mwenye kipaji chake. Ilikuwa ni hatari kila mara kuhamia klabu kwa matumaini ya kushinda taji kubwa la soka la klabu za Ulaya, kwa kuwa PSG bado wana kazi katika maendeleo.

Kylian Mbappe, Edinson Cavani, na Adrien Rabiot ni wachezaji wa kiwango cha dunia, waliokuwa chini ya kocha, Unai Emery, lakini hakutosha kuweka mambo yote pamoja. Uwezo wa walio uwanjani ni mzuri vya kutosha kusaidia PSG kuvuka Ligi ya Ufaransa, lakini dhidi ya Real Madrid ilikuwa ni shida.

Kwa bahati mbaya, ni klabu hii ambayo wengi walifikiri Neymar angejiunga naona mazungumzo kuhusu kuhamia Madrid hayajakoma tangu ahamie Ufaransa.

### #4. ANTOINE GRIEZMANN (ATLETICO MADRID)

Chaguo hili lazima litanguliwe kwa kusema kwamba Griezmann amekuwa na mafanikio makubwa tangu alipowasili Atletico Madrid. Amekuwa nyota wao, akifunga mabao mengi muhimu.

Uhamisho, hata hivyo ulitajwa zaidi ya msimu mmoja, haswa kwa Barcelona, na kwa sababu alibaki Atletico ili kuwasaidia wakati wa kuzuiliwa kwa uhamisho, lakini akahamia Camp Now.

Mtindo wake kwa urahisi, unafaa zaidi timu hiyo. Ni mpiga chenga maridadi, mwenye uwezo mzuri wa kuunganisha na alikuwa vizuri pamoja na Lionel Messi, Luis Suarez, na Ousmane Dembele.

Wakati Atletico ilipotwaa taji la ligi msimu wa 2013/2014, sehemu kubwa ya mafanikio ilitokana na yeye.

Alipotua Barcelona hakuwa na mafanikio yale ambayo aliyapata kule Atletico na akalazimika kurudi alikotoka ambako anacheza hadi sasa.

### #5. DANIEL STURRIDGE (PERTH GLORY FC)

Kesi ya Sturridge inakuwa chungu. Ilipobainika kuwa wakati wake Liverpool ulikuwa umekamilika, ambapo alihamia kwa mkopo mnamo Januari ilikuwa muhimu sana, haswa katika mwaka wa Kombe la Dunia.

Katika uchaguzi kati ya Newcastle United ya Rafael Benitez na Alan Pardew ya West Brom, alichagua upande wa pili, na wengi walishangazwa na chaguo lake. Katika mechi yake ya tatu pekee, aliumia msuli wa paja dhidi ya Chelsea na alikaa nje kwa wiki mbili.

Akiwa fiti kabisa, aliunda ushirikiano wa ajabu na Luis Suarez msimu wa 2013/2014, na mabao yake 21 ya ligi yalistahili medali ya ubingwa.


Lakini stori ya Sturridge kwa sasa ni tofauti kabisa, mambo yamegeuka haraka sana na kila kitu sasa kimebakia kuwa historia.

## Nukuu

"Kila kitu ni tofauti. Kujithamini, hali ya akili na kujiamini. Kocha mpya amewasili na amefanya mabadiliko mengi. Xavi ameingiza falsafa ambayo alikuwa amedumisha kwa miaka mingi, sisi ni timu kamili zaidi sasa, tunafanya mambo mengi vizuri. Ni wazi kwamba bado tuna safari ndefu, lakini hii ndiyo njia," **Kiungo wa kati wa Barcelona, Sergio Busquets akiamini kuwa 'Blaugrana' hao wamekuwa timu "kamili" zaidi chini ya mchezaji mwenzake wa zamani na bosi wa sasa, Xavi Hernandez.**



"Kwangu mimi, lilikuwa chaguo bora zaidi kucheza na kufurahia soka tena. Nilipoteza kidogo huko Manchester kwa sababu sikuwa nikicheza. Ninajisikia vizuri sana hapa Sevilla. Jiji ni nzuri sana na sisi ni timu nzuri kwa hivyo, kwangu, ni kamili. Ninacheza kwa hivyo ninafuraha, lakini nipo hapa hadi mwishoni mwa msimu ndivyo ilivyo," **mshambuliaji wa Manchester United, Anthony Martial anayecheza kwa mkopo Sevilla**



"[Pierre-Emerick] Aubameyang ni zawadi kutoka peponi, yeye ni mchezaji mzuri ambaye mara zote huingia kwenye chumba akiwa katika hali nzuri na huzoea haraka mazingira mapya," **Kocha wa Barcelona, Xavi, baada ya mshambuliaji huyo wa zamani wa Arsenal, kufunga bao la nne wakati wakishinda 4-0 dhidi ya Osasuna hivi karibuni hilo likiwa ni la sita kwake katika mechi tisa alizocheza.**





# NONDO 5 ZA HAYATI MAGUFULI MICHEZONI

**Na Adam Fungamwango**

MACHI 17, Tanzania iliadhimisha mwaka mmoja kamili tangu kuondokewa na Rais wa awamu ya tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, aliyefariki dunia siku hiyo wakati akipigania uhai wake katika Hospitali ya Mzena, Dar es Salaam. Ni rais pekee nchini aliyefia madarakani.

**Pamoja na kazi zingine, lakini Dk. Magufuli alikuwa ni mpenda michezo, akipata muda alikuwa anakwenda uwanjani kuungana na Watanzania wenzake.**

Kama itakumbukwa Machi 8, mwaka juzi alipokuwa mgeni rasmi kwenye mechi ya Ligi Kuu msimu wa 2019/20, kati ya Yanga na Simba.

Kwenye mechi hiyo, Yanga ilishinda bao 1-0, lililowekwa wavuni na Bernard Morrison, wakati huo akiichezea timu hiyo, kabla ya kuhamia Simba miezi michache baadaye.

Alionekana pia kufuatilia mambo mbalimbali ya michezo. Alijua vitu vingi kuhusu michezo mbalimbali, kiasi cha kushangaza wengi wanaposimama na kuiongelea.

Haya ni baadhi ya mambo aliyoyasema wakati wa uhai wake michezoni, akiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania...

#### #1. AWAPASHA WANG'OA VITI

Akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari mwaka 2016, ikiwa ni mwaka mmoja baada ya kuingia madarakani, pamoja na mambo mengine, alionyesha kukasirishwa na mashabiki waliodhaniwa kuwa ni wa Simba kwa kung'oa viti kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, wakati huo ukiitwa wa Taifa.

Akasema kuwa pamoja na mambo mengine ya kufanya, anapenda sana michezo, lakini hapendi kuona watu wakivunja viti.

"Napenda michezo, lakini sipendi kuona timu zinang'oa viti. Bora nikaangalie Ndondo Cup kuliko kwenda kuangalia timu zikifungwa zinang'oa viti," alisema Magufuli.

Alisema hayo kutokana na tukio lililotokea Oktoba Mosi mwaka 2016, Ligi Kuu msimu wa 2015/16, Yanga ilipocheza na Simba kwenye uwanja huo.

Ni bao la Mrundi Amissi Tambwe ndilo lililoleta kizazaa kwani kabla ya kufunga, Tambwe aliutengeneza mpira kwa mkono na kisha kuuweka wavuni, kitu kilicholalamikiwa na mashabiki wengi wa Simba uwanjani na kuanza kufanya vurugu, hadi pale Shiza Kichuya alipoisawazishia.

#### #2. AITAKA SIMBA ITWAE KOMBE LA AFRIKA

Ilikuwa ni Mei 9, kwenye Uwanja wa Taifa (sasa Mkapa), Rais Magufuli wakati huo alipoitwa kuikabidhi Kombe la Ubingwa wa soka nchini 2017/18.

Katika mechi hiyo, Simba ilifungwa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar. Hakuridhika na aina ya soka la mabingwa lilivyokuwa linachezwa.

Akasema kabisa kuwa haoni kikosi cha kwenda kupambana kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, na kuwataka wabadilishe kikosi na kusajili baadhi ya wachezaji wenye uwezo.

"Mimi kama kiongozi wenu nitafurahi sana siku moja mkiniita hapa kuja kukabidhi Kombe la Afrika litakalochukuliwa na timu yoyote katika nchi yetu. Kwa hiyo niwaombe Simba mkawe wa kwanza basi kuleta Kombe la Afrika hapa Tanzania." Alisema maneno hayo, mara baada ya mechi hiyo.

#### #3. AIOMBA MOROCCO KUJENGA UWANJA NCHINI

Mwaka 2016, Rais Magufuli, pamoja na mambo mengi, alimuomba Mfalme wa Morocco kujenga uwanja mkubwa wa kisasa jijini Dodoma.

Akiwa kwenye ziara ya siku tano nchini, Hayati Magufuli aliomba serikali ya nchi hiyo kuijengea Tanzania uwanja ambao utafanya watu wengi kuendelea kupenda na kufuatilia michezo

"NimemWomba Mfalme ajenge msikiti mkubwa hapa jijini Dar es Salaam. Lakini nimemwomba atujengee uwanja mkubwa wa mpira Dodoma ambao utakaogharimu kiasi cha dola milioni 100 ambao utakuwa mkubwa zaidi ya huu wa taifa, vyote amekubali atajenga," amesema Rais Magufuli.

#### #4. AIJIA JUU STARS KWA KUFUNGWA

Ilikuwa ni Oktoba 2018, alipowaita viongozi wa Shirikisho la Soka nchini (TFF) na wachezaji wa timu ya Taifa, Taifa Stars Ikulu, Dar es Salaam.

Hiyo ilikuwa ni baada ya ushindi dhidi ya Cape Verde wa mabao 2-0, Stars ikisaka tiketi ya kwenda AFCON iliyofanyika mwaka 2019 nchini Cameroon.

Katika hafla hiyo, Magufuli alionekana kuchukizwa na tabia ya kufungwafungwa ovyo.

"Napenda sana michezo, lakini mimi siyo shabiki wa timu yoyote hapa Tanzania. Sipendi kushindwa, na ni aibu sana watu milioni 55 kushindwa kutinga AFCON," alisema.

#### #5. ATANGAZA KUJENGA UWANJA DODOMA

Novemba mwaka juzi, Magufuli akiwa kwenye sherehe za kuapishwa aliahidi kujenga uwanja mkubwa mjini hapo kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma.

"Naishukuru na kuipongeza kamati ya maandalizi kwa matayarisho mazuri kwa hakika sherehe imefana sana, kwa sababu watu wamejaa ndani ya uwanja, lakini wamejaa pia nje ya uwanja, hii inanipa changamoto serikali nitakayoianza na kwamba kitu cha kwanza tutaanza kujenga uwanja mkubwa sana hapa Dodoma, ili sherehe zingine zitakapokuja watu wote wa Dodoma waweze kuwa ndani ya uwanja na washerehekee vizuri," alisema.

**JE, WAJUA?**



KWA miaka 64 sasa, Pele bado ndiye mchezaji anayeshikilia rekodi ya kufunga hat-trick kwenye Kombe la Dunia akiwa na umri mdogo zaidi. Nyota huyo wa zamani wa Brazil alitupia hat-trick hiyo mwaka 1958 akiwa na umri wa miaka 17.



# THTU yamwomba Rais Samia mambo manane

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHAMA cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU), kimemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuyatafutia ufumbuzi mambo manane ikiwamo nyongeza ya mshahara aliyoahidi kwa wafanyakazi mwaka huu.

Sambamba na hilo, kimetaja mambo saba ambayo yamefanywa ya serikali chini ya uongozi wa Rais Samia ndani ya mwaka mmoja ikiwamo upandishwaji wa madaraja kwa watumishi wengi wanaostahili.

Mwenyekiti wa THTU Taifa, Dk. Paul Loisulie, ndiye aliyeyataja mambo hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mwaka mmoja wa Rais Samia kwa wafanyakazi hao.

Dk. Loisulie alisema wafanyakazi wana matumaini makubwa na Rais Samia atazitafutia ufumbuzi kero zao ambazo wameziwasilisha kwa maandishi kwa Katibu Mkuu Kiongozi mwishoni mwa mwaka 2021.

"Katika andiko hilo tulilowasilisha, tulichambua kwa kina kila suala kwa kuonyesha chanzo chake, madhara, namna ya kutatua na tija itakayopatikana baada ya kutatuliwa, baadhi ya masuala hayo ni malalamiko juu ya marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma kuhusu muda wa kustaafu watumishi wanataaluma," alisema.

Alisema malalamiko yaliyojitokeza kwa watumishi wa umma yanayolenga Waraka wa Msajili wa Hazina namba sita wa mwaka 2015 ambao unaleta athari kubwa kwa mishahara ya wafanyakazi waendeshaji wa mkondo wa PGSS.

"Kukosekana kwa Sheria ya Kazi na miongozo ya serikali inayoweka viwango vya mishahara katika sekta binafsi ya Taasisi za Elimu ya Juu, masuala yaliyobakia kupatiwa ufumbuzi katika Bodi ya Mikopo likiwamo suala la ushirikishaji wa vyama vya wafanyakazi kwenye Bodi ya Bodi ya Mikopo ya wanafunzi Elimu ya Juu (HESLB) na mengine machache,"alisema.

Pia alitaja mambo mengine ni ucheleweshwaji wa mafao kwa waastaafu, kukosekana kwa fao la huduma ya afya baada ya kustaafu na kusitishwa kwa nyongeza ya mwaka ya mshahara kwa watumishi.

"Pia mabadiliko ya Sheria ya Utumishi wa Umma ambayo inaleta athari kwa taratibu za nidhamu kwa watumishi wa umma kwa sababu ya matumizi mabaya,"alisema.

Kuhusu nyongeza ya mishahara, mwenyekiti huyo alisema ilikwama kwa miaka sita sasa na wana matumaini lipo ndani ya uwezo wa Rais Samia kutokana na kauli aliyoitoa mwaka jana wakati wa sherehe za Mei Mosi mkoani Mwanza kwamba ambapo aliahidi nyongeza kwa mwaka huu.

"Sisi wafanyakazi kwa tunaunganisha nguvu zetu za sala na dua kwa mama ili aweze kutafuna fupa hili sugu, tunaamini liko ndani ya uwezo wake na Mungu yupo pamoja nae, zipo faida nyingi za kuongeza mishahara kwa wafanyakazi kijamii, kisiasa na kiuchumi," alisema.

Akizungumzia mafanikio, Dk. Loisulie alisema Rais Samia ameondoa mateso ya Bodi ya Mikopo ulio watesa wafanyakazi kwa miaka kadhaa kwa kuondoa tozo ya kutunza thamani ya mkopo ambayo ilikuwa inaongeza mkopo kila mwaka badala ya kupunguza.

Pia alisema kupungua kwa kiburi cha madaraka kwa wakuu na watendaji wa taasisi, kuongezeka kwa amani na utulivu ofisini mwa wafanyakazi kutokana na mabadiliko hayo. "Awali, wafanyakazi wengi walikuwa katika hali ya uoga na njia panda kutokana na vitisho, pia kufufuka kwa matumaini ya maboresho ya mishahara iliyosimamishwa kupandishwa kwa miaka mitano iliyotangulia, hii ni baada ya kutoa ahadi ya kuboresha maslahi ya mishahara katika sherehe za Mei Mosi jijini Mwanza mwaka 2021," alisema.

Dk. Loisulie alisema kuendelea kulipwa malimbikizo ya mishahara na maslahi mengine kwa awamu mbalimbali na kuongeza kwa umri wa wanufaika wa Bima ya Afya kutoka miaka 18 hadi 21.



Mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) mwaka pili, James Ndizu (kushoto), akionyesha wageni kazi zake anazofanya chuoni hapo, ikiwa ni sehemu ya masomo yake. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Chana ahimiza weledi, ufanisi kwa watumishi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Pindi Chana, amewataka watumishi wa umma kufanya kazi kwa uweledi, ufanisi na kuzingatia taratibu na kanuni zilizoko ili kutoa huduma bora kwa jamii.

Chana alitoa kauli hiyo alipokuwa akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa ofisi hiyo kilichokuwa kikipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/22 na makadirio ya Bajeti Mwaka 2022/23.

Aliwataka kuwa wabunifu katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku na kuhudumia umma kama inavyokusudiwa na serikali.

Alisema kwamba lengo la kuanzishwa kwa mabaraza ya wafanyakazi ni kuongeza ufanisi na tija katika sehemu za kazi, waajiri na wafanyakazi kubadilishana mawazo na kubaini mbinu mbalimbali za kukabiliana na kero zinazowakabili.

"Nimefarijika kuona upendo na mshikamano uliopo kati ya menejimeti na wafanyakazi wote wa ofisi hii idara zote na upande wa sera kwa kweli nawapongeza sana na moyo huu wa kazi mlionao unajenga heshima ya Ofisi ya Waziri Mkuu," alisisitiza.

# Wazazi wanaume watajwa chanzo ukatili kwenye jamii

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMATI za Mpango Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) umebaini moja ya chanzo cha ukatili katika jamii kwa sasa, ni wazazi wa kiume kukimbia na kutelekeza familia zao kutokana na hali mbaya ya uchumi.

Mwakilishi wa Shirika la Watoto la New Light Children Center Organization (NELICO), Kwaresma Manko, alitoa hoja hiyo jijini hapo kwenye mkutano wa wadau wa kupinga ukatili ulioandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP),wenye lengo la kujadili robo ya pili ya utekelezaji wa mpango huo.

Manko alisema kutokana na hali hiyo, ni vyema vijana kupewa mafunzo ya namna ya kutunza familia zao, ikiwamo kujifunza ujasiriamali ambao utawasaidia kujiinua kiuchumi na kuepuka adha ya kutelekeza watoto na familia kwa ujumla.

"Ni vema vijana wakapewa semina ya namna ya kutunza watoto wao, wakifanya hivyo itachangia kupunguza ukatili kwa wanawake na watoto,"alisema Manko.

Alisema wao kama wadau wa kutokomeza ukatili wa kijinsia wamekuwa wakitoa elimu kwa vijana ya namna ya kupambana na ukatili wa kijinsia katika maeneo mbalimbali yanayowazunguka.

Kwa upande wake, Ofisa Habari wa TGNP, Jackson Malangalila, alisema lengo la mkutano huo ni pamoja na kuangalia utekelezaji wa robo ya pili ya mradi wa kutokomeza ukatili wa kijinsia unaotekelezwa katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

"TGNP kama taifa tunatekeleza mpango wa taifa wa kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto ndio maana tumeandaa mkutano huu

kwa asasi 25 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini," alisema Malangalila.

Alisema wanafanya hivyo ili kujua asasi nyingine zinakumbana na kero zipi katika utekelezaji wa mpango huo ili kuzifanyia ufumbuzi.

Malangalila alisema wamekuwa wakizijengea uwezo kamati za kutokomeza ukatili namna ya kujikinga pale wanapokutana na kesi za ukatili, ambazo

zinamalizwa kifamilia mitaani.

Naye Immaculate Deus kutoka asasi ya kupinga ukatili ya The Voice Marginalized Community (TVMC), alisema matatizo wanayokumbana nayo katika mapambano ya kupinga ukatili ni pamoja na utelekezaji wa kesi na mila na desturi katika familia mbalimbali.

Alisema familia nyingine zinamaliza kesi za ukatili wa kijinsia kifamilia na kupelekea watoto wa kike kushindwa kupata haki zao msingi, kutokana na wahusika unawawia vigumu k ufuatilia kutokana na kukosa ushirikiano kutoka kwa ndugu.





# Ma-DC, wakurugenzi wapewa muda wa kukamilisha vituo huduma za afya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAZIRI Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, amewaagiza wakuu wote wa wilaya na wakurugenzi kusimamia kikamilifu ujenzi wa vituo vya afya, zahanati na hospitali ili ifikapo Aprili 30, majengo yote yawe yamekamilika.

Bashungwa alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki, alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Igawilo iliyoko Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Alisema kasi ya ujenzi katika wilaya na halmashauri katika baadhi ya halmashauri hairidhishi kwa sababu fedha za ujenzi tulipeleka maeneo yote.

"TAMISEMI tunaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo hususani kwenye eneo la afya msingi, tulipokea fedha awamu ya kwanza kwa ajili ya kujenga vituo vya afya 233 kwenye maeneo ya kimkakati na vinajengwa kwa fedha zetu sisi wenyewe Watanzania," alisema Bashungwa.

Aliongeza kuwa katika awamu ya kwanza serikali ilipokea Sh. bilioni 58.2 kwenye vituo 233 na kwamba kila kituo kilipata Sh. milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje, maabara na kichomea taka.

Alisema vipo vituo ambavyo vilipokea fedha hizo kati ya Oktoba hadi Desemba na kwamba hivyo vinatakiwa kukamilika hadi kufikia Aprili 30, mwaka huu.

Alisema mkuu yeyote wa wilaya na mkurugenzi atakayeshindwa kukamilisha kabla ya tarehe 30 atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Aliongeza kuwa hadi kufika Februari 15, 2022 vituo 110 kati ya 233 vilivyopokea fedha vilikuwa vimekamilika na kwamba vituo hivyo vilivyokamilika vilikwishapelekewa fedha ya awamu ya pili, hivyo Sh. bilioni 27.5 zilitolewa ili kuendeleza ujenzi wa majengo ya wodi ya wazazi, upasuajі, kufulia na njia ya kutembea.

"Serikali yetu inavyotujali fedha zilizotengwa katika bajeti ya maendeleo ya ruzuku ya ndani kwa mwaka wa 2021/2022 shilingi bilioni 113.7 zilikwenda kwenye vituo vya kutolea huduma kwa Hospitali za Wilaya 104, jumla ya bilioni 66.3 kwa ajili ya kuendeleza na kukamilisha ujenzi wa hospitali hizo ambazo zilianza kujengwa mwaka 2018/2018 na 2019/2020," alisema Bashungwa.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alimhakikishia Waziri Bashungwa kuwa ujenzi wa Hospitali ya Igawilo pamoja na vituo vingine utakamilika kabla ya muda uliopangwa.

Alisema kwa sasa ujenzi wa hospitali umefikia asilimia 95, umebaki ukamilishaji wa baadhi ya majengo na vifaa tiba.



Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Juma Kipanga, juzi, akipima moja ya madirisha yaliyojengwa katika Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) cha Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya wakati wa ziara yake ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa chuo hicho, ambacho kinagharimu zaidi ya Sh. bilioni mbili. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# VETA yaagizwa kukamilisha ujenzi wa vyuo

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

NAIBU Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Juma Kipanga, amewataka wasimamizi wote wa ujenzi wa vyuo vya Mamlaka ya Ufundi Stadi (VETA) kuweka mpango kazi ambao utasaidia kufuatilia kwa karibu ujenzi wa vyuo hivyo ili vikamilike kwa wakati na vianze kutumika.

Kipanga alitoa kauli hiyo juzi alipotembelea ujenzi wa Chuo cha VETA Wilaya ya Mbarali, ambao unaendelea, hivyo aliwasisitiza wataalamu kuweka mpango kazi ambao utawaongoza kufanya ununuzi ya vifaa vya ujenzi, ratiba ya kukamilisha na kubaini mahitaji.

Alisema wakati wa ukaguzi wa mradi wa ujenzi wa chuo hicho alibaini kutokuwapo kwa mpango kazi ambao huenda ungekuwapo shughuli za ujenzi wa chuo hicho ungekamilika mapema.

"Nawaomba wataalamu mnaosimamia ujenzi wa chuo hiki hakikisheni mnazingatia mpango kazi wa umaliziaji ambao utawaongoza kutambua mahitaji ya vifaa, muda wa kumaliza shughuli na kiasi cha fedha kitakachotumika kununua vifaa hivyo utaratibu huu utazaa matunda mkiuzingatia," alisema Kipanga.

Aidha, Kipanga alieleza kuwa ili ujenzi wa Chuo cha VETA Mbarali ukamilike, lazima wazingatie mpango wa umaliziaji wa kila jengo huku ukibainisha kazi zinazofanyika na kubandika taarifa ya nini kinaendelea katika kila jengo.

Alisema ujenzi wa chuo hicho unatakiwa kukamilika Machi 31, mwaka huu, tayari kwa ajili ya kupokea wanafunzi wa fani mbalimbali ambayo wametuma maombi ya kujiunga na chuo hicho.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Ruben Mfune, alimhakikishia Naibu Waziri Kipanga kwamba wataongeza kasi ya usimamizi wa mradi huo ili kufika Machi 31 tayari wawe wamekabidhi mradi huo.

Alimshukuru Waziri Kipanga kwa kutembelea mradi huo na kufanya ukaguzi wa hatua kwa hatua na kisha kukagua majengo yote ili kujiridhisha na hatua mbalimbali zilizofikiwa katika ujenzi huo.

Aliiomba VETA kukamilisha haraka ujenzi huo, na kwamba atakuwa anafanya ukaguzi wa mara kwa mara chuoni hapo ili kujua hatua zilizofikiwa katika ukamilishaji na kuanza kuwanufaisha wananchi wa Mbarali.

Ofisa Elimu Mkoa wa Mbeya, Ernest Hinju, alisema jumla ya wanafunzi 3,000 wamechaguliwa kujiunga na mafunzo ya ufundi stadi, na kwamba chuo cha Mbarali nacho kitapatiwa wanafunzi kadhaa ili kupata ujuzi wa masuala mbalimbali.

## Ileje yapewa mil.100 /- za mikopo

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

JUMLA ya shilingi milioni 100 zimekabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ileje mkoani Songwe kwa ajili ya mikopo kwa vikundi vya wajasiriamali.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa utoaji wa mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri zote nchini.

Hundi hiyo ilikabidhiwa na Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Anna Gidarya, kwenye stendi ya basi Itumba wakati wa kuadhimisha mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan. Fedha hizo zinahusisha pia mikopo ya pikipiki 10 na bajaji mbili.

Gidarya alisema serikali imetoa mikopo ya bajaji na pikipiki kwa lengo la kuwasaidia vijana kujikwamua kiuchumi ili waweze kumudu mahitaji yao.

Aliwataka vijana kuvitunza vyombo hivyo ili vidumu na viweze kurejesha mikopo iliyotolewa na halmashauri hiyo ambapo jumla ya vijana 12 walinufaika.

"Hakikisheni mnazingatia sheria za usalama barabarani pamoja na kujiepusha na ubebaji wa bidhaa za magendo kwa sababu atakayebainika atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria ikiwa ni pamoja na usafiri wake kutaifishwa," alisema.

Upande wake Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Ileje, Rodrick Sengela, alisema kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, halmashauri hiyo ilitenga kiasi cha fedha zaidi ya Sh. milioni 84 kwa ajili ya vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu.

Alisema hadi sasa halmashauri imefanikiwa kutoa mikopo ya zaidi ya Sh. milioni 90 na kwamba wataendelea kivinufaisha vikundi mbalimbali vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ambavyo vitakidhi vigezo vinavyohitajika.

Aliwataka wanufaika wote kuhakikisha mikopo yao wanairejesha kwa wakati ili iweze kuwanufaisha na wengine, lengo likiwa kila mjasiriamali anakuza biashara yake.






Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleyman Abdullah (katikati), akikata utepe kuashiria uzinduzi wa maandalizi ya mashindano makubwa ya Qu'raan Tukufu Afrika ya 22 yatakayofanyika Aprili 17, yalioandaliwa na Taasisi ya Al- Hikma Foundation jijini Dar es Salaam jana. Wapili kushoto ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya mashindano hayo, Shekh Nurdin Kishk na Rais wa taasisi hiyo, Shekh Sharif Abdulkadir (wanne kulia). **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mambo muhimu kuendeleza rasilimali haya

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo, Othman Masoud Othman, amesema maarifa na uongozi bora ni mambo muhimu yanayohitajika katika kuendeleza rasilimali zilizoko Zanzibar ili ziweze kuleta manufaa na maendeleo ya watu wote nchini.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar alitoa kauli hiyo katika maeneo tofauti akiwa katika ziara ya kichama kutembelea majimbo ya uchaguzi Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema Zanzibar inauwezo mkubwa wa kuwezesha kila mwananchi kuishi maisha bora yenye neema yanayotokana na uendelezaji wa rasilimali za nchi zilizoko ikiwamo ardhi, lakini muhimu pia kuwapo viongozi wanaowajibika kwa watu.

Alisema kwamba iwapo rasilimali za ardhi zitatumika kwa kupewa wawekezaji na wamiliki wakapewa fidia ndogo, huku mwekezaji akifaidika na biashara anayoifanya haisaidii kuwafaidisha wananchi na badala yake ni jambo linalochangia kuongeza umaskini kwa wananchi.

Alisema duniani kote serikali ikiihitaji ardhi kwa shughuli za maendeleo ya wananchi, mmiliki hulipwa fidia, lakini iwapo kuna shughuli za uwekezaji kibiashara hakuna sababu mwananchi kutofaidika vyema na rasilimali hiyo.

Alisema kwamba Zanzibar inahitaji kutengeneza viongozi wanaowajibika kwa watu na wenye nidhamu na Zanzibar itaweza kufikia mahala pazuri kimaendeleo na kuleta neema kwa watu wote.

Aliongeza kuwa iwapo suala la uongozi bora na maarifa ya aina ya kuwajibika kwa watu yatatumika ipasavyo, upo uwezekano mkubwa kwa vijana wote nchini kutengenezewa na kupata ajira katika kuendeleza jitihada za kiuchumi na kuleta maendeleo yao na taifa kwa jumla.

Alisema Chama cha ACT- Wazalendo kinaamini katika ustawi bora wa watu wote nchini, na kwamba jambo kubwa linalohitajika ni imani na dhamira njema kwa viongozi na wenye maarifa bora zinaopaswa kutumika katika kuendeleza rasilimali kwa maisha yenye neema kwa kila mwananchi wa Zanzibar.

Akizungumzia suala la Muungano, alisema aina ya sasa ya muungano ulivyo unaunufaisha upande mmoja zaidi, huku Zanzibar ikikosa fursa mbalimbali muhimu zinazotokana na muungano.

Naye mjumbe wa Kamati Kuu wa Chama hicho, Ismail Jussa Ladhu, aliwataka wanachama na wananchi kuungana katika jitihada za kupigania maendeleo ya Zanzibar sambamba na kutetea muungano kwa Zanzibar na bara kuwa na hadhi sawa.

Alisema mfumo wa sasa wa muungano uliopo hauwezi kusiadia Zanzibar kujibadilisha kisera na kuweka mfumo bora wa kuleta maendeleo ya kiuchumi kwa Wazanzibari kutokana na vyanzo vingi vya kimaendeleo kudhibitiwa na upande mmoja wa muungano.

# Kongamano la uwekezaji maji kuleta fursa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maji, Nishati na Madini, Shaib Hassan Kaduara, amesema kongamano la kitaifa la maji lililofanyika hivi karibuni litapunguza pengo la uwekezaji wa maji sio kwa Zanzibar pekee bali kwa bara zima la Afrika.

Kaduara alitoa kauli hiyo wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, kuhusu kongamano la kitaifa la uwekezaji wa maji lililofanyika Visiwani Zanzibar wiki iliyopita.

Alisema uwekezaji katika sekta ya maji utarudisha mahitaji ya kiuchumi na kijamii katika kanda za Afrika.

Alifahamisha kuwa Zanzibar imekuwa na miradi mingi ya maji ambayo ikifadhiliwa na tasisi mbalimbali ulimwenguni, lakini tatizo la maji limekuwa sugu na muda mwengine sababu zinatokana na ukosefu wa wataalamu wa maji, lakini utaalamu wa miundombinu iliyokuwapo.

Aidha, alisema lengo la kufanya kongamano hilo Zanzibar ni kuwakutanisha na kuitangaza sekta ya maji na kuipa kipaumbele sekta hiyo ambayo ina umuhimu mkubwa kwa wananchi wa Zanzibar.

Akizungumzia kuzinduliwa kwa programu maalum ya maendeleo ya maji 'Zanzibar Water Investment Program', alisema programu hiyo ni ya kwanza iliyoundwa chini ya programu ya uwekezaji wa maji barani Afrika (AIP) ambayo inalenga kukusanya dola bilioni 30 kwa mwaka kuelekea usalama wa maji barani Afrika.

Alisema lengo la mpango huo ni uendeshaji endelevu na wakuaminika wa upatikanaji wa majisafi na salama ambao utachangia ustawi wa kiuchumi nchini na kuleta maendeleo kwa wananchi katika mipango ya kitaifa na kutoa muelekeo mzuri katika sekta hiyo.

Waziri Kauduara alisema ni matumaini yake kwamba washirika wa maendeleo wataiunga mkono serikali katika utekelezaji wa mpango huo.

Aidha, Waziri Kaduara alisema wizara anayoiongoza ina miradi mbalimbali ya maji ambayo itaweza kupunguza tatizo la maji katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar na kuwashauri wananchi kuendelea kushirikiana na kuwa wazalendo katika kulipia huduma hiyo.

Alikemea tabia inayofanywa na watu ya kuharibu miundombinu ya maji na kusisitiza kuwa serikali haitakuwa na muhali watu hao katika kuharibu miundombinu ya maji na badala yake watachukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani.

Naye Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Mgereza Miraji Mzee, alisema wanapitia miradi yote iliyoanzishwa kuanzia mwaka 1990 hadi mwaka 2020 katika sekta ya maji kwa ajili ya kubaini mafanikio na changamoto katika sekta hiyo.

# TAMWA yampa tano Rais Mwinyi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA)-Zanzibar, kimepongeza uamuzi wa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kuunda wizara maalum itakayoshughulikia masuala ya wanawake, hivyo kuwa wizara inayojitegemea, nje ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kama ilivyokuwa awali.

Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema hali hiyo itapelekea masuala ya wanawake kushughulikiwa kwa makini zaidi ikiwamo kutengewa rasilimali inazostahiki ili kuhakikisha mipango, utekelezaji na ufuatiliaji unafanyika kama inavyostahiki.

"Pendekezo la kuwa na wizara za wanawake pekee, lilikuja katika mikutano ya kimataifa ya wanawake hasa uliofanyika Nairobi mwaka 1985 kufuatia dhuluma ambazo wanawake wamekumbana nazo na zilivyowafanya kuwa nyuma katika nyanja za kimaisha, hivyo wizara ya wanawake pekee ilishauriwa ili inyanyue hali hizo za wanawake duniani kwa ujumla na nchi zinazoendelea kwa upekee hasa kama Zanzibar ambayo imezongwa zaidi na mifumo kandamizi dhidi ya wanawake na watoto wa kike," alisema Dk. Mzuri.

Alisema pia TAMWA inampongeza Waziri Riziki Pembe aliyeteuliwa kuiongoza Wizara hiyo kutokana na uwezo wake na uzoefu, hivyo anaamini kuwa ataweza kuleta mabadiliko yanayostahiki.

Alimshauri waziri huyo kuweka mifumo madhubuti ya kurikodi maendeleo ya wanawake katika nyanja za kiuchumi na kiuongozi kwa vile hazijaratibiwa vizuri.

"Hivi sasa kuna jitihada nyingi za kuinua kipato cha wanawake, lakini bado hakuna mifumo mizuri kuonyesha hasa mabadiliko yanayotokea na mapungufu yaliyoko ili hatua zaidi ziweze kuchukuliwa. Kukiwa na takwimu maalum za wanawake hao itakuwa ni rahisi kuonyesha maendeleo yaliyofikiwa katika kundi hilo muhimu ambalo linafanya zaidi ya asilimia 50 ya wakazi wote wa Zanzibar," alisema.

Dk. Mzuri alisema pia katika uongozi, takwimu za wanawake katika nafasi mbalimbali za kiutendaji katika ngazi za kitaifa na shina zikiwamo kwenye wakurugenzi, miundo ya bodi, kamati za kiutendaji bado ni changamoto kuzipata pamoja na kuwa nchi inatekeleza itifaki na maazimio mbalimbali ya kuleta usawa wa kijinsia hasa katika uongozi.

"Itifaki ya Umoja wa Afrika (AU) ya mwaka 2003 na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ya mwaka 2008 zote zinahimiza asilimia 50/50 katika vyombo vya maamuzi katika nyanja zote hizo bila ya takwimu na mikakati maalum haitakuwa rahisi kupima mwelekeo wa nchi katika hilo," alisema.

# Corona ilivyopaisha manunuzi mitungi ya oksijeni Muhimbili

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema kipindi ulipoingia mlipuko wa UVIKO-19, Hospitali ya Taifa Muhimbili ililazimika kununua takribani mitungi ya oksijeni 600 kwa siku, huku mmoja kulingana na ujazo ukiuzwa kati ya Sh. 20,000 hadi 40,000.

Kabla ya mlipuko wa ugonjwa huo, unaosababishwa na virusi vya corona, hospitali hiyo ilikuwa ikinunua mitungi ya oksijeni takribani 250 hadi 300 kwa siku kutoka kwa kampuni za watu binafsi.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, baada ya kuzindua chanzo cha kuzalisha hewa tiba 'oxygen generating plant' kilichojengwa kwa ufadhili wa Korea Foundation for International Health Care (KOFIH), katika Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, mkoani Dar es Salaam.

Alisema kuwapo kwa chanzo hicho kunaipunguzia gharama serikali ambayo ilitumia takribani Sh. milioni 175 kwa siku kununua mitungi ya oksijeni, akiishukuru KOFIH, na kuagiza kwamba Hospitali ya Mloganzila itaanza kujiendesha yenyewe kuanzia Julai mwaka huu, kutoka usimamizi wa MNH.

"Wakati wa UVIKO-19 mitungi ilinunuliwa hadi 600 kwa siku. Mtambo huu utaokoa fedha nyingi pia ni biashara tutawauzia na watu binafsi. Nimeelezwa tangu uanze kutumika Januari mwaka huu hadi Machi, Mloganzila imeuza mitungi takribani 1,500 kwa MNH.

"Nimeshapeleka barua kwa katibu mkuu kwamba muanze kujitegemea kutoka Hospitali ya Muhimbili. Mloganzila imekuwa tayari inastahili ijitegemea, sasa itaamuliwa iitwe jina gani jipya, kulingana na uongozi. Pia maombi ya kuwaongezea bajeti nitayafanyia kazi," alisema Ummy.

Alisema kwamba MNH itaendelea kubaki katika hadhi yake ya kuhudumia kitaifa na pia akibainisha matarajio ya kuanza kuifanyia ukarabati kutokana kuanza kutoa huduma miaka mingi, bila maboresho ya kina.

Awali, Naibu Mkurugenzi MNH, Dk. Julieth Magandi, alisema Mloganzila pekee, ilitumia takribani Sh. milioni 33 kila mwezi kwa ajili ya kununua mitungi ya oksijeni kutoka kwa wazabuni binafsi, akisema iwapo wa mtambo huo ni fursa kibiashara na ukuaji wa mapato.




Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), Hamisi Amiri (wanne kulia), pamoja na wahitimu wa kozi ya usalama katika viwanja vya ndege inayotolewa na Chuo cha Usafiri wa Anga Tanzania (CATC) wakiwa pamoja na uongozi wa chuo hicho, katika mahafali yaliyofanyika chuoni hapo. Watatu kutoka kushoto ni Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Huduma wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Teophory Mbilinyi na Kaimu Mkuu wa Chuo cha Usafiri wa Anga Tanzania (CATC), John Ndimbo (wapili kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sekta ya fedha yaimarika, nchi kufunguka

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan madarakani, sekta ya kibenki imeelezwa kuimarika na kuwa imara, salama, tulivu na yenye faida hali iliyoleta mazingira wezeshi kwa wananchi.

Aidha, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ameeleza kuwa nchi imefunguka kiuchumi na mzunguko wa fedha umeimarika hasa baada ya serikali kuhakikisha fedha za bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22 zilizopitishwa na Bunge zinafika kwa wingi kuhudumia jamii.

Hayo yalibainishwa katika kongamano la kutimiza siku 365 madarakani kwa Rais Samia Suluhu Hassan lililofanyika katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) Jumamosi.

Ofisa Mkuu wa Fedha Benki ya NMB, Juma Kimori, alisema katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia madarakani sekta ya benki ilishuhudia kukua kwa mizania kwa asilimia 24 hadi kufikia jumla ya mali ya Sh. trilioni 38.7, kiasi ambacho ni rekodi kwenye sekta hiyo.

Alifafanua kuwa, sekta ya benki nchini kwa ujumla iliendelea kuwa imara na yenye mtaji wa kutosha. Kwa upande wa faida, kutokana na kasi madhubuti ya mapato, pamoja na kuimarika kwa ubora wa mikopo, benki zote nchini kwa ujumla zilipata faida kabla ya Kodi ya Mapato ya Sh. trilioni 1.04.

"Hii ni faida ya juu zaidi katika historia ya sekta ya kibenki kwa hapa nchini. Haya yote ni matokeo ya utendaji wako wa kipekee na wa kizalendo pamoja na serikali yako ndani ya mwaka mmoja tu wa urais wako," alisema Kimori.

Kwa upande wake, Dk. Tulia alieleza kuwa kumekuwapo na mazingira wezeshi na rahisi kwa wananchi kujiinua kipato kutokana na shughuli mbalimbali zinazofanyika za kiuchumi, lakini huduma muhimu za kijamii ikiwamo afya, maji, umeme na miundombinu kupatikana kirahisi na uhakika.

"Tunapiga hesabu kwa maana ya yale yaliyofanyika kwa mwaka mmoja, kwenye eneo la afya asilimia 62.32 ya fedha zilizotengwa na Bunge katika bajeti zimeshafika maeneo husika, unaweza kuona ni nusu mwaka, lakini ameshavuka nusu ya lengo.

"Upande wa maji asilimia 76.51 ya fedha zilizotengwa zimeshafika kwenye maeneo husika, hizi takwimu nazitaja mpate picha ili ikifika mwezi Juni mwaka huu mjue itafika wapi kwa sababu kazi inaendelea na kuzidi," alisema Dk. Tulia.

Kwa upande wa maliasili asilimia 58.08 ya fedha zimeshafika, sekta ya ujenzi ni asilimia 60.69, sekta ya uchukuzi ni asilimia 23.32, sekta ya elimu ni asilimia 69.31.

Aidha, kwa upande wa TAMISEMI ambayo imegusa maeneo mengi alisema ni asilimia 39.46, kwa upande wa mikoa yote asilimia 56.03.

"Kwa ujumla ukifanya tathmini na sekta nyingine unapata wastani wa asilimia 60.5 kutoka Julai 2021 hadi Januari 2022, kwa hivyo Rais Samia anaifanya kazi inaendelea ameweza na kuzidi," alisema Dk. Tulia.

Kimori awali alieleza kuwa katika mwaka mmoja wananchi wameshuhudia mipaka ya nchi ikifunguka na sasa biashara za kimataifa zimezidi kuongezeka na kwamba Watanzania wengi wamepata fursa za kufanya biashara nje ya nchi na kukuza uchumi.

# Ajali nyingine yaua wawili yajeruhi 17

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WATU wawili wamefariki dunia akiwamo dereva baada ya gari walilokuwa wakisafiria aina ya Coaster likitokea Dar es Salaam kuelekea Dodoma kuligonga lori kwa nyuma katika eneo la Oil Com, Nanenane, barabara kuu ya Morogoro-Dar es Salaam, Mjini Morogoro.

Muuguzi kiongozi wa zamu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Joyce Kiwale, akizungumza kwa niaba ya Mganga Mkuu wa hospitali hiyo, alikiri kupokea majeruhi 17 wa ajali hiyo kuanzia saa 11.15 alfajiri jana na wawili kati yao ambao ni wanaume walipoteza maisha wakati wakipatiwa matibabu.

Kiwale alisema miongoni mwa majeruhi hao, watatu ambao pia ni wanaume wamelazwa kutokana na kupata majeraha ya kuvunjika na wengine wamepata matibabu na kuruhusiwa kuondoka.

Ilidaiwa miongoni mwa waliofariki dunia wamo dereva na utingo wa gari hiyo aina ya Coaster.

Alisema ajali iliyohusisha basi la abiria mali ya kampuni ya Ahmeed na lori lililokuwa likisafirishwa kuelekea nchini Congo, iliyotokea eneo la Melela Kibaoni Darajani wilayani Mvomero, katika barabara kuu ya Morogoro-Iringa, iliyopoteza maisha ya watu 23 na wengine 26 kujeruhiwa, mmoja wa majeruhi Ali Athumani alisema dereva wa coaster alilokuwa amepanda alikuwa mwendo kasi kutaka kulipita Fuso lililokuwa mbele na kukutana na gari jingine ilipojaribu kurudi kushoto ghafla na aliligonga Fuso.

Majeruhi wengine Msafiri Msafiri na Juliana John kwa nyakati tofauti walisema tangu walipoanza safari kutoka Dar es Salaam, dereva wa gari hiyo alikuwa katika mwendo kasi na walishtuka kusikia kelele za abiria baada ya ajali.

Juliana alisema baada ya ajali walipata msaada wa haraka kutoka kwa wasamaria wema na askari wa Jeshi la Polisi, huku yeye akipata majeraha madogo mwilini.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro SACP Fortunatus Musilim, alipotafutwa kwa njia ya simu, alikiri kutokea kwa ajali hiyo na chanzo ni lori lililokuwa limeharibika na kuegeshwa barabarani bila kuwekwa alama za tahadhari.

Waandishi wa habari waliofika eneo la ajali walikuta Coaster pekee ikiwa eneo hilo na namba zake za usajili zilifunikwa kwa kitu kinachosadikiwa ni tope na kushindwa kunukuu namba zake.

Hata hivyo, katika hali isiyokuwa ya kawaida, Mganga Mkuu wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Dk. Daniel Nkungu, alikataa kutoa kibali kwa waandishi wa habari kupiga picha majeruhi wa ajali hiyo kwa madai kuwa wamezuiwa kufanya hivyo baada ya tukio la kusambaa kwa picha ya aliyekuwa Mbunge wa Mikumi, Joseph Haule, maarufu Prof. J, akiwa chumba cha wagonjwa mahututi.

MAKALA MAALUM

# Diplomasia ya China inafuata uelekeo sahihi wa historia

**MHE. Chen Mingjian,** Balozi wa China nchini Tanzania

WAKATI wa mikutano mikuu miwili ya kila mwaka (Bunge la Taifa na Mkutano wa Mashauriano ya Kisiasa ya Watu wa China), Waziri wa Mambo ya Nje wa China anafanya mkutano unaofuatiliwa kwa ukaribu na waandishi wa habari ili kutambulisha sera ya mambo ya nje ya China na maoni na mapendekezo yake kuhusu hali ya kimataifa na masuala yaliyogusa hisia, akitoa tafsiri ya kina ya uhusiano wa China na ulimwengu wa nje. Tarehe 7 Machi mwaka huu, Mjumbe wa Baraza la Taifa na Waziri wa Mambo ya Nje Wang Yi alifanya mkutano na waandishi wa habari tena na kujibu maswali 27 kutoka kwa vyombo vya habari vya China na vya nje katika muda wa dakika 100, akizungumzia mabadiliko ya sasa ya uhusiano wa kimataifa, na kuelezea kwa uwazi sifa pekee, utume na mwelekeo wa diplomasia ya China.

**I. Kudumisha imara amani na maendeleo ya ulimwengu na kulinda usawa na haki kimataifa**

Ulimwengu unapitia mabadiliko makubwa ambayo hayajaonekana katika karne moja. Wakati janga la UVIKO-19 likiendelea kuibuka, mzozo wa Ukraine unaibuka. Je, China inaweza kuleta utulivu zaidi na nguvu chanya kwa ulimwengu wenye mashaka? Katika maneno yake yenye ufasaha, Mjumbe wa Baraza la Taifa Wang Yi aliuambia ulimwengu kwamba China itatunza ahadi yake na kutimiza matarajio yake ya awali, kuheshimu ahadi zake, na kuendelea kujenga amani ya dunia, kuchangia maendeleo ya kimataifa na kulinda utaratibu wa kimataifa.

Kuhusu hali ya Ukraine, zingatio la mtizamo wa kimataifa, Mjumbe wa Baraza la Taifa Wang Yi alifafanua kwa mara nyingine msingi wa msimamo wa China, akisema kwamba China itajitegemea katika kutathmini hali hiyo na kutoa msimamo wake kwa misingi ya ustahili wa suala hilo. Huku akitoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kuzidisha juhudi za kukuza mazungumzo ya amani, Wang Yi alipendekeza "mpango wa mambo sita" wa China kuhusu kuzuia mgogoro mkubwa wa kibinadamu nchini Ukraine. Alitangaza kuwa Chama cha Msalaba Mwekundu cha China kitaipatia Ukraine sehemu ya vifaa vya dharura vya kibinadamu haraka iwezekanavyo.

Katika masuala mengine yaliyovuta hisia, Mjumbe wa Baraza la Taifa Wang Yi alitoa wito kwa pande zote zinazohusika kufuata kanuni ya "Afghan-led and Afghan-owned" kusaidia watu wa Afghanistan katika Kilindi cha matatizo, alisisitiza kuwa uwezo wa kulinda usalama na maendeleo katika Mashariki ya Kati lazima urejeshwe kikamilifu kwa watu katika eneo hilo, na kuzitaka pande zinazohusika kukutana katikati kutafuta suluhu ya kisiasa ya masuala ya Peninsula ya Korea. Haya yote yanathibitisha kikamilifu kwamba China, ikiwa ni mjumbe wa kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na nchi kubwa inayowajibika, daima imekuwa ikishikilia maono ya pamoja, ya kina, ya ushirika na usalama endelevu, na ilichukua jukumu linalofaa katika kulinda amani na utulivu wa dunia.

Mpango wa Ukanda na Njia (BRI) na Mpango wa Maendeleo Ulimwenguni (GDI) ni mipango mikuu ya ushirikiano iliyowekwa na Rais Xi Jinping. Ni bidhaa muhimu za umma zinazochangiwa na China kwa ajili ya ushirikiano wa maendeleo ya kimataifa. Hadi sasa, familia ya BRI ina wanachama 180, na GDI imepokelewa kwa shauku na kuungwa mkono na UN na karibu nchi 100.

Mjumbe wa Baraza la Taifa Wang Yi alisisitiza kuwa China itafanya kazi na jumuiya ya kimataifa ili kufikia ushirikiano wa ngazi ya juu, ufanisi bora wa gharama, usambazaji bora wa hali ya juu na ustahimilivu wa maendeleo, ili kuufanya Mpango wa Ukanda na Njia kuwa "ukanda wa maendeleo" kwa manufaa ya dunia. Alisema China itafanya kazi na pande zote katika maeneo manne ili kutekeleza mpango wa GDI hatua kwa hatua: Kwanza, kuendeleza ushirikiano katika maeneo yaliyopewa kipaumbele; Pili, kukabiliana na mahitaji ya nchi zote; Tatu, kushirikiana na taratibu za ushirikiano; Nne, kuwafikia washirika wa sekta zote. China itafanya kazi na nchi nyingine zote ili kuhakikisha kwamba hakuna nchi au mtu binafsi anayeachwa nyuma na hakuna matarajio yanayopuuzwa, ili kujenga kwa pamoja jumuiya ya maendeleo ya kimataifa.

Wakati utaratibu wa kimataifa unakabiliwa na changamoto ambazo hazijawahi kushuhudiwa na utawala wa kimataifa unakumbwa na mkanganyiko, tunapaswa kufanya nini? Jibu lililotolewa na Mjumbe wa Baraza la Taifa Wang Yi ni kuimarisha mshikamano na ushirikiano chini ya bendera ya ushirikiano wa pande nyingi na kujenga kwa pamoja jumuiya yenye mustakabali wa pamoja wa wanadamu. Alisema ni lazima tushikilie msimamo wa pande nyingi, kutetea maadili ya kawaida ya utu, kulinda mfumo wa kimataifa na Umoja wa Mataifa katika msingi wake, kuzingatia kanuni za msingi zinazoongoza mahusiano ya kimataifa kwa kuzingatia madhumuni na misingi ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa, na kufanya kazi kwa ajili ya haki na mfumo wa utawala wenye usawa zaidi duniani. Ili kuongoza mageuzi ya mfumo wa utawala wa kimataifa na dhana ya usawa na haki, China imekuwa ikisonga mbele kwa ujasiri.



Mh. Chen Mingjian, Balozi wa China nchini Tanzania. **PICHA: MTANDAO**

**II. Kuimarisha uongozi wa Chama cha Kikomunisti cha China na kulinda kwa uthabiti maslahi ya taifa na furaha ya watu.**

Chama cha Kikomunisti cha China (CPC) ni uti wa mgongo wa watu wa China na nguzo ya diplomasia ya China. Mjumbe wa Baraza la Taifa Wang Yi alisema kuwa kusimulia vizuri hadithi za ustawi wa CPC na kuwasilisha, kutetea na kuendeleza jina zuri la CPC ni kazi muhimu na jukumu muhimu ambalo huduma ya kidiplomasia ya China inapaswa kutekeleza. Kadiri nchi nyingi zaidi zinavyotumaini kujifunza kuhusu siri za mafanikio ya CPC, tutaendelea kuwasilisha simulizi za CPC vizuri ili marafiki wengi zaidi wa kimataifa waweze kuelewa CPC, na jumuiya ya kimataifa iweze kuiona CPC kupitia lenzi angavu zaidi.

Akijibu majaribio ya baadhi ya nchi ya kuishambulia China kwa kisingizio cha "kukuza demokrasia", Mjumbe wa Baraza la Taifa Wang Yi alisisitiza kuwa demokrasia ya watu katika mchakato wote wa China ni demokrasia pana, halisi na yenye ufanisi, ambayo inafurahia kuidhinishwa kwa moyo wote na kuungwa mkono na watu wa China pamoja na kutambuliwa kote ulimwenguni. Demokrasia katika nchi tofauti inapaswa kuchanua kama maua tofauti, na kudhani kuwa kuna mfumo mkamilifu usio na makosa sio tu kinyume na ari ya demokrasia, lakini inaashiria maafa kwa demokrasia.

"Kuwahudumia watu na kutatua matatizo yao" ni wajibu wa huduma ya kidiplomasia ya China." Huu ni muhtasari wa kina wa madhumuni na utume wa diplomasia ya China na Mjumbe wa Baraza la Taifa Wang Yi. Mnamo mwaka 2021, kwa kufuata kanuni inayozingatia watu, China iliandaa shughuli za uokoaji wa dharura baada ya mabadiliko ya ghafla ya hali ya Ukraine, ilitoa chanjo kwa mamilioni ya raia wa China wanaoishi katika nchi 180 dhidi ya UVIKO-19, kushughulikia kesi zaidi ya 60,000 za msaada kwa raia wake wanaoishi nje, na ilifanikiwa kuokoa makumi ya raia wa China waliotekwa nyara. Mwaka 2022, China itajikita zaidi katika kuunda jukwaa la huduma bora za kibalozi, kujenga mfumo wa ulinzi wa raia wa China na masilahi yao nje ya nchi, na kuzindua mpango wa kuwezesha usafiri salama na usiozuiliwa, ili kulinda maisha na masilahi halali ya Wachina wa ng'ambo.

**III. China itakuwa daima mwanachama wa dunia inayoendelea, na kusimama bega kwa bega na marafiki wa Afrika**

China ndiyo nchi kubwa zaidi inayoendelea duniani. Kuimarisha mshikamano na ushirikiano na idadi kubwa ya nchi zinazoendelea ni chaguo thabiti la kimkakati ambalo China imefanya. Katika mkutano na waandishi wa habari, Mjumbe wa Bazara la Taifa hilo Wang Yi alijibu maswali ya vyombo vya habari mfululizo kuhusu uhusiano wa China na nchi za ASEAN, nchi za Asia ya Kati, Afrika, Amerika ya Kusini na nchi za visiwa vya Pasifiki ya Kusini. Majibu yake yametuma ujumbe mzito kwamba China itakuwa daima mwanachama wa nchi zinazoendelea na mshirika wa dhati na wa kutegemewa wa nchi zinazoendelea. Mwaka huu, China itachukua uenyekiti wa BRICS kama fursa ya kuunganisha zaidi sauti na nguvu za masoko yanayoibukia na nchi zinazoendelea, na kusaidia kufanya utaratibu wa kimataifa kuwa wa haki na usawa.

Uhusiano kati ya China na Afrika daima umo katika ajenda ya mkutano na waandishi wa habari wa Waziri wa Mambo ya Nje wa China wakati wa mikutano mikuu miwili ya kila mwaka. Hii inaonyesha kikamilifu umuhimu wa uhusiano kati ya China na Afrika katika diplomasia ya China. Mjumbe wa Baraza la Taifa Wang Yi alisema kuwa kwa miaka mingi, China imejenga zaidi ya kilomita 10,000 za reli, hadi kilomita 100,000 za barabara kuu, karibu bandari 100, na hospitali na shule zisizohesabika - Afrika, akisisitiza kwamba hii sio "mitego ya madeni" bali alama ya ushirikiano. Akibainisha kuwa mwaka huu China na nchi za Afrika zimeanza kutekeleza yale yaliyotolewa na Mkutano wa Nane wa Mawaziri wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika (FOCAC), Wang Yi alisema kuwa China itaheshimu ahadi yake ya kushirikiana na Afrika, kutetea ari ya urafiki wa China na Afrika na ushirikiano, na kufanya kazi na mataifa ya Afrika kutekeleza "programu tisa" za ushirikiano na Afrika zilizotangazwa na Rais Xi Jinping.

Mjumbe wa Baraza la Taifa Wang Yi alipendekeza vipaumbele vitatu vya ushirikiano wa China na Afrika mwaka huu. Kwanza, China itaendeleza kwa nguvu ushirikiano wa kupambana na UVIKO na Afrika, kutimiza kikamilifu ahadi ya Rais Xi Jinping ya kutoa dozi bilioni moja za chanjo kwa bara hilo, na kusaidia Afrika kuongeza uwezo wa uzalishaji wa chanjo barani humo. Pili China itaunganisha GDI na Ajenda 2063 ya Umoja wa Afrika na kuchukua hatua madhubuti kusaidia ufufuaji wa uchumi na maendeleo endelevu ya Afrika. Tatu, China itachukua hatua kuhusu matazamio ya amani na maendeleo katika pembe ya Afrika, na kuchukua jukumu muhimu kwa ajili ya amani na maendeleo ya Pembe ya Afrika na Bara la Afrika kwa ujumla.

HABARI MICHEZO

# AISHA AAHIDI MABAO ULAYA

Na Adam Fungamwango

STRAIKA wa Timu ya Yanga Princess na timu ya Taifa ya Soka ya Wanawake, Twiga Stars, Aisha Masaka, ambaye amepata dili la kwenda kucheza soka la kulipwa nchini Sweden kwenye Klabu ya BK Hacken FF, amesema hatowaangusha Watanzania, badala yake anakwenda kufanya kazi ambayo amechukuliwa kwa ajili ya kuifanya, nayo ni kufunga mabao.

Masaka ambaye ndiye kinara wa ufungaji wa Ligi Kuu ya Wanawake msimu uliopita, akipachika mabao 35, alisema hayo juzi baada ya kuagwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, kabla ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Yanga na KMC.

"Nilipoambiwa kwa mara ya kwanza nilijisikia furaha sana, na mara nyingi nafasi kama hizi zikipatikana hazitakiwi kufanyiwa mzaha kwa sababu hutokea mara chache, mimi nakwenda na naahidi sitowaangusha Watanzania, kwa sababu sisi tunaopata nafasi hizi tunatakiwa tukajitume na kuwa na nidhamu ili kuwatengenezea mazingira mazuri wengine ambao wamebaki nyumbani.

"Wakiona Watanzania wanajituma na wana nidhamu, watakuja tena kuchukua wachezaji wengine, tunataka wachezaji wanawake tuwe wengi kutoka Tanzania tunaocheza mpira wa kulipwa, kwa maana hiyo hata wanaobaki nyumbani pia wapambane, wawe na nidhamu, wasikilize makocha wao, hakuna kinachoshindikana chini ya jua," alisema mchezaji huyo.

Mchezaji huyo anaondoka, akiiacha timu yake ya Yanga Princess ikiwa msimu huu haipo kwenye kiwango kizuri kwenye Ligi Kuu, lakini amesema kazi inayompeleka huko ni kufunga mabao tu.

"Wamenichukua kwa sababu wanasikia na kuona mimi nafunga, kwa hiyo najua kazi yangu kubwa niliyochukuliwa ni kufunga," alisema.

Timu hiyo inayocheza Ligi Kuu Sweden, ilikuwa mabingwa mwaka 2020, na msimu huu ilitolewa na Machester City kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa upande wa wanawake.



NI WEWE?...



Rais mstaafu wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jakaya Mrisho Kikwete, akisalimiana na mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, kabla ya mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na Yanga kushinda 2-0. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAVA yaja na Nyerere National Tour

Na Saada Akida

UONGOZI wa Kamisheni ya mchezo wa Wavu wa Ufukweni Tanzania (TAVA), umeandaa shindano lijulikanalo kama Nyerere National Tour, linalotarajiwa kufanyika Machi 26 hadi 27, mwaka huu katika Fukwe za Palumboreef- Uroa, zilizoko Zanzibar.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa TAVA, Ford Edward, alisema TAVA imeandaa shindano hilo ambalo kwa mwaka huu litafanyika katika mikoa tofauti wakianzia visiwani Zanzibar.

Alisema hadi sasa mataifa manne yamethibitisha kushiriki mashindano hayo ikiwamo Tanzania ambayo ni mwenyeji, Burundi, Kenya na Algeria.

"Shindano hilo litashirikisha timu zote za wanaume na wanawake na tayari Tanzania wanatoa wachezaji 18, wanaume 10 na nane wanawake, Burundi na Kenya kila moja itatoa wachezaji wa kiume wawili na idadi kama hiyo wakike kike huku Algeria wao wakitoa wachezaji wa kiume pekee," alisema Ford.

Alisema kuna faida ya wachezaji kushiriki shindano hilo la wazi mojawapo ikiwa ni kuwawezesha kupata alama zitakazowasaidia kupata nafasi ya kushiriki michuano mikubwa zaidi ya kidunia kwa sababu kuna mashindano hadi ufikishe kiasi cha alama fulani ndio utaweza kushiriki.

"Kamisheni ya Wavu tumedhamiria kuwaletea wachezaji wetu shindano hapa nyumbani ili pia kuepuka gharama za kutafuta alama nje ya nchi, lakini kuutangaza utalii wetu pamoja na kuukuza mchezo wetu," alisema Mwenyekiti wa huyo wa TAVA.

Alisema mashindano hayo yapo katika Kalenda ya Shirikisho la mchezo huo duniani na inafahamika mwishoni mwa Machi kuna shindano linafanyika ambalo wameamua kulipa jina la Nyerere National Tour.

"Kwa sasa tunaanza na Zanzibar baada ya hapo tutaangali ni sehemu gani ya Tanzania kupeleka, naomba wachezaji kutumia mashindano hayo kuongeza pointi kabla ya kuelekea katika mashindano makubwa pamoja na wadhamini kujitokeza kusaidia kukuza mchezo huu," alisema Ford.

## Minziro awawashia moto wachezaji

Na Dennis Fussi

KOCHA wa Geita Gold, Fred Minziro, amewajia juu wachezaji wake baada ya kupoteza mechi mbili mfululizo za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizunguma na gazeti hili, kocha huyo amesema kuna wachezaji ndani ya timu yake wanaonekana kama wameridhika na sasa wanashindwa kujituma kuipigania timu jambo ambalo hataki kuliona.

"Geita tuna malengo yetu na hatuwezi kuyafikia kama kuna wenzetu wachache wanashindwa kutimiza majukumu yao kitu ambacho ni kibaya na mimi sitokubali kiendelee," alisema Minziro.

Geita iliyopo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa ligi hiyo, hivi karibuni ilipoteza dhidi ya Yanga na Mtibwa Sugar, matokeo ambayo hayajamfurahisha kocha huyo, aliyeipandisha daraja.

## Mlela sasa achonga kutupia kwa Mkapa

Na Adam Fungamwango

MSANII maarufu wa filamu na tamthilia nchini, Yusuph Mlela, amesema amepata furaha kubwa kufunga bao kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na kuweka historia katika maisha yake, kwani wapo mastraika wengi Tanzania wanaocheza Ligi Kuu hawajawahi kufunga bao kwenye dimba hilo.

Mlela alisema hayo juzi baada ya kumalizika kwa mechi ya utangulizi kati ya timu ya Wasanii na Viongozi wa Yanga iliyoisha kwa Wasanii kuchapwa mabao 2-1.

"Kiukweli nimefurahi sana, nimeweka historia kubwa kwenye maisha yangu, hasa kwenye soka, sikuwahi kutegemea kitu kama hiki, unajua kuna mastraika wengi wanaocheza timu mbalimbali za Ligi Kuu hawajawahi kufunga bao kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, lakini mimi nimefunga. Sifanyi tu mazoezi ya nguvu, lakini kama nafanya, halafu napata nafasi ya kucheza, nina uwezo wa kucheza Ligi Kuu," alisema Mlela.

Kuhusu ushabiki wa soka, alisema yeye ni mpenzi wa Yanga, na alianza kuishabikia tangu miaka ya mwanzoni mwa 1990.

Ilikuwa ni mechi ya utangulizi kabla ya mechi ya Ligi Kuu kati ya Yanga na KMC, timu ya Wasanii ikiundwa na wachezaji filamu, tamthilia, lakini wale wa muziki wa bongo fleva.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### POGBA RADA ZA BARCA

KIUNGO wa kati wa Manchester United, Paul Pogba (29), amerejea katika darubini ya Barcelona baada ya klabu hiyo ya Hispania kusaini mkataba mnono wa udhamini. Mkataba wa kiungo huyo wa kimataifa wa Ufaransa kwenye Uwanja wa Old Trafford unakamilika msimu huu wa majira ya joto. ***(Star)***

### RUDIGER KUTUA JUVE

MLINZI wa Ujerumani, Antonio Rudiger, ambaye mkataba wake katika klabu ya Chelsea unamalizika msimu huu wa majira ya joto na amekubali kujiunga na Juventus kwa mkataba wa miaka minne. ***(La Gazzetta dello Sport, via Mail)***

### HAALAND KUMNG'OA JESUS

JUVENTUS watamnunua mshambuliaji wa Manchester City na Brazil, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 24, ikiwa klabu hiyo ya England itafanikiwa kumsajili mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21 kutoka Borussia Dortmund. ***(Star)***

### NEWCASTLE NA NEYMAR

KLABU ya Newcastle United inataka kumsajili mshambuliaji nyota wa Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 30, ambaye mkataba wake na Paris St-Germain unamalizika mwaka 2025. ***(Fichajes, via Teamtalk)***

### CESAR SAFI BARCELONA

NYOTA wa Chelsea, Cesar Azpilicueta amekubali kujiunga na Barcelona kwa uhamisho huru. Mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania mwenye umri wa miaka 32, unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Football Insider)***

### JORGINHO AITAKA SERIE A

WAKALA wa kiungo wa kati wa Chelsea, Jorginho amesema mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia mwenye umri wa miaka 30, anataka kurejea Ligi Kuu Italia, Serie A. ***(Mirror)***

### BOUNOU ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inatathmini uwezekano wa kumnunua golikipa wa Morocco na Sevilla, Yassine Bounou mwenye umri wa miaka 30. ***(Mirror)***

### NUNEZ AWINDWA ATLETICO

KLABU ya Atletico Madrid inamtaka sana mshambuliaji wa Uruguay mwenye umri wa miaka 22, Darwin Nunez, ambaye ameisaidia Benfica kufuzu robo fainali ya Mabingwa Ulaya. ***(Fichajes)***


### MESSI HAONDOKI PSG

LIONEL Messi hana nia ya kuondoka PSG na anapanga kukamilisha mkataba wake wa miaka miwili aliosaini na klabu hiyo ya Ufaransa. ***(Marca)***

### DEMIRAL ANUKIWA UNITED

MANCHESTER United wanamtaka mlinzi wa Uturuki mwenye umri wa miaka 24, Merih Demiral, ambaye yuko Atalanta kwa mkopo kutoka Juventus. ***(Fanatik)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# XAVI: MESSI ANAWEZA KURUDI TENA BARCELONA

●●● Milango ipo wazi kabisa, muda wote mimi nitakapokuwa kocha hapa, akitaka kuja kila siku...

**BARCELONA,** Hispania

XAVI ameeleza kuwa Barcelona mara zote watamkaribisha tena Lionel Messi wakati yeye akiendelea kuwa kocha wa 'Blaugrana' hao.

**Messi aliondoka Barca mwaka jana katika hatua ambayo ilishangaza ulimwengu wa soka, huku miamba hao wa Hispania wakishindwa kumudu kutimiza masharti ya mkataba mpya ambayo yote yalikuwa yamekubaliwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34.**

Hiyo ilimaanisha Messi aondoke kama mchezaji huru na akajiunga na Paris Saint-Germain, ingawa uhamisho wake kwenda mji mkuu huo wa Ufaransa bado haujafikia kilele kilichotarajiwa.

PSG wanatazamia kunyakua taji la Ligue 1, lakini waliangukia pua kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kufungwa na Real Madrid katika hatua ya 16-bora, taji ambalo wamekuwa wakilisaka kwa udi na uvumba.

Messi, ambaye aliukosa mchezo wa PSG dhidi ya Monaco kutokana na kuugua, amefunga mabao saba pekee katika michuano yote.

Hata hivyo, pamoja na Kylian Mbappe, anaongoza kwenye chati ya pasi za mwisho za Ligue 1 akiwa na 10 hadi sasa, huku nafasi zake 48 alizotengeneza zikimfanya kuwa mchezaji mbunifu zaidi katika kikosi cha PSG kwenye Ligi Kuu Ufaransa.

Kumekuwa na uvumi kwamba Messi anaweza kuondoka PSG mwishoni mwa msimu huu na ingawa inaonekana kwamba Paris watakuwa tayari kumpoteza yeye na Mbappe, ambaye mkataba wake unamalizika na akionekana kujiunga na Madrid.

Na sasa Xavi hatakataa nafasi ya kuunganishwa tena na mchezaji mwenzake huyo wa zamani, iwe kama uhamisho wa kustaajabisha au kama mgeni tu.

"Messi milango ipo wazi kabisa Barca," alisema Xavi akiwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wa jana, Jumapili wa El Clasico dhidi ya Real Madrid.

"Muda wote mimi nitakapokuwa kocha hapa, akitaka kuja kila siku kutazama mazoezi au kuzungumza na kocha anakaribishwa, ni mchezaji bora kabisa katika historia.

"Anastahili heshima kubwa kutoka kwa klabu. Lakini Leo ana mkataba na PSG, nadhani alisaini wa miaka miwili."

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
TENERIFE
VERSUS
ALMERIA
1 | 2.41
X | 3.13
2 | 2.89

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# NEWCASTLE YAMFUNGIA KAZI NEYMAR



**NEWCASTLE,** England

KLABU ya Newcastle ya Ligi Kuu England, inafikiria kumsajili kwa donge nono nyota wa Paris Saint-Germain, Neymar da Silva Santos Júnior msimu wa majira ya joto.

Mshambuliaji huyo wa Brazil pamoja na Lionel Messi, walizomewa na mashabiki wa timu yao wakati wa mchezo wa Ligue 1 walioshinda mabao 3-0 dhidi ya Bordeuaux licha ya yeye Neymar kufunga la pili.

Kwa sehemu alilaumiwa katika kipigo cha mabao 3-1 kutoka kwa Real Madrid na PSG kuondolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ripoti zinaeleza kuwa Neymar anasemekana kukata tamaa na anafikiria kuondoka msimu wa majira ya joto unaokuja.

Newcastle sasa wanatafakari kuhusu 'fursa ya dhahabu' kumhamishia Ligi Kuu England mmoja wa mchezaji bora zaidi duniani kwa pauni milioni 200.



## Saka ataka unyenyekevu Arsenal

**LONDON,** England

BUKAYO Saka amesisitiza kuwa Arsenal lazima "wabaki wanyenyekevu" licha ya kuimarisha matumaini yao ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao baada ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Aston Villa, Jumamosi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England, alifunga bao hilo pekee - likiwa ni la 2,000 kwa 'Washika-bunduki' hao kwenye Ligi Kuu- wakati walijiimarisha hali yao kwenye nne bora, na kuwa mbele kwa pointi nne dhidi ya Manchester United walioko nafasi ya tano.

Kikosi hicho cha kocha Mikel Arteta sasa kimeandikisha ushindi wa ugenini mara tano mfululizo kwenye Ligi Kuu kwa mara ya kwanza tangu Mei 2015.

Saka alidumisha kiwango chake cha kuvutia akiwa ugenini, akiwa amehusika katika mabao sita kwenye mechi tano za mwisho za ligi nje ya dimba la Emirates, akifunga matano na kusaidia moja.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, alipongeza juhudi za ulinzi za wenzake wakati wakiona ushindi mwingine muhimu, huku akiwataka kuendelea kujitahidi kufikia malengo yao.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDE

# MWALIMU MONDULI ASHINDA MIL. 5/- JACKPOT BONUS SPORTPESA

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Mto wa Mbu, Wilaya ya Monduli mkoani Arusha, Ivory Samford Shao, ameshinda shilingi 5,344,009, kama bonasi ya Jackpot ya Sportpesa ya wiki iliyopita, baada ya kupatia kwa usahihi mechi 11 kati ya 13.

**Akizungumza baada ya makabidhiano ya hundi katika Ofisi za Sportpesa jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Shao alisema alianza kucheza na Sportpesa kuanzia mwaka 2018, baada ya kuona matangazo kwenye TV na mitandao ya kijamii.**

“Nilianza kucheza Sportpesa miaka minne iliyopita baada ya kuona matangazo na habari za Jackpot kwenye TV, hivyo na mimi nilivutiwa kutaka kujaribu bahati yangu kama wengine.

“Unajua mimi ni mwalimu wa michezo, nafundisha shule ya msingi, hivyo napenda sana kufuatilia mambo yote ambayo yana asili ama nasaba na michezo jambo ambalo kwangu ilikuwa kazi rahisi sana,” alisema.

Akielezea namna alivyopata ushindi huu wa bonasi alisema Jumanne na Jumatano aliweka mkeka wake baada ya kushauriana na baadhi ya walimu wenzake akaona wala haina haja ya kuchelewa, hivyo akaweka ubashiri wake mapema.

“Jackpot hii niliyoshinda niliweka jumla ya mikeka 2, mmoja Jumanne na mwingine Jumatano. Nikiwa maskani siku ya Jumanne majira ya saa 12 alikuja daktari na kunikuta nacheza drafti akaniambia Jackpot ya Sportpesa imefika zaidi ya bilioni moja,” alisema.

Shao alisema Jumamosi mpaka kufika usiku mkeka mmoja ulikuwa umeshatoa timu saba na hivyo aliingia Jumapili akiwa anasubiria matokeo ya timu tano zilizosalia.




Mshindi wa Bonasi ya Jackpot ya SportPesa, Ivory Samford Shao, kutoka Monduli mkoani Arusha, akionyesha mfano wa hundi ya Sh. 5,344,009 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 11 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. Jackpot inayoshindaniwa wiki hii ni Sh. 1,042,431,860. **PICHA: SPORTPESA**

“Unajua siku ya Jumapili ilianza kwa mimi kuangalia mechi ya Simba wakati mechi ile inaendelea ndipo na mechi za Wolves, Rennes na nyingine nazo zilianza kuchezwa. Nilikuwa na kitete kidogo kwa sababu ushindi haukuja moja kwa moja. Ilibidi kusubiria baadhi ya mechi mpaka muda wa nyongeza ndio timu kupata matokeo.”

Alisema baada mechi kumalizika, alirudi kijiweni anapocheza drafti na kuwaambia ‘washkaji’ zake mkeka wake umepata bonasi ya timu 10, hivyo wakati wanajadiliana meseji kutoka Sportpesa ya kumtaarifu juu ya ushindi iliingia.

Ivory anawashauri Watanzania wacheze bila kuchoka kwani Jackpot ya Sportpesa imeiva na itapata mshindi muda wowote. “Mimi najitahidi kucheza kadiri niwezavyo, naipigania hii bilioni moja kwa nguvu zote”.

Aidha, alisema fedha alizozipata atawekeza kwenye biashara yake na kubwa atanunua vifaa kwa ajili ya wanafunzi wake na nyingine atatumia na familia. Kwa upande wa SportPesa, Meneja Uhusiano na Mawasiliano, Sabrina Msuya alianza kwa kumpongeza kwa ushindi wake: “Ivory ameonyesha juhudi mbali na kuufahamu mpira wa miguu, kazi yake ya ualimu imemsaidia kuweza kuchanganua mechi mbalimbali.

“Jackpot bado inaendelea na sasa imefika Sh. 1,042,431,860, hivyo basi ni wakati mwafaka kwa Watanzania kuwa mabilionea,” alisema Sabrina.

# Moallin aanza kuona mwanga Azam FC

**Na Dennis Fussi**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Abdihamid Moallin, amesema wachezaji wake wanatakiwa kujitoa na kujituma katika michezo ijayo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, kama ambavyo wamefanya katika mechi dhidi ya Namungo na Somalia.

Azam ilipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Namungo na juzi Jumamosi waliibuka na ushindi wa 3-1 dhidi ya timu ya Taifa ya Vijana chini ya umri wa miaka 23 ya Somalia katika mchezo wa kirafiki uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

Mabao ya Azam FC yalifungwa na Ayoub Lyanga dakika ya 64, Idris Mbombo dakika ya 81 na Shaaban Iddi Chilunda dakika ya 90 na ushei.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Moallin alisema sasa anaiona timu yake inaanza kuimarika katika ari na upambanaji kwa wachezaji wake kitu ambacho walikikosa kwenye michezo mitatu iliyopita.

“Hiki ndicho tulikuwa tunakikosa katika mechi tatu zilizopita, lakini leo (juzi), tumethibitisha ugenini. Tumeanza na Namungo FC ugenini na sasa Somalia,” alisema Moallin.

“Mechi zote zilikuwa ngumu, lakini tumepigania alama tatu.

“Sasa natarajia kuona mechi zijazo wachezaji wangu wanajitoa kupambana kutafuta pointi muhimu michezo iliyoko mbele yetu ili kufikia malengo ya timu,” alisema kocha huyo.

Alisema katika mechi tatu zilizopita dhidi ya Polisi waliyoshinda bao 1-0, dhidi ya Coastal Union waliyotoka suluhu na kisha kufungwa 2-0 dhidi ya Biashara, hawakucheza katika kiwango cha kuvutia.

“Unaweza kuona kwenye mechi tatu tulipata pointi nne tu, tulifungwa, tukashinda na kutoka sare, na wachezaji hawakuwa kwenye kiwango bora sana, lakini sasa naanza kuona ari kubwa kwao.”

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

“1” - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
“X” - NI TIMU KUTOKA SARE
“2” - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 21/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3241 | FC Tuapse vs FC Forte Taganrog | 2.70 | 3.10 | 2.75 |
| 13:00 | 4825 | FC Yessentuki vs Anzhi Makhachkala | 14.46 | 7.33 | 1.12 |
| 14:00 | 2896 | Sile Yildizspor vs Antalya Kestelspor | 1.68 | 3.37 | 4.82 |
| 14:00 | 5246 | Tiddim Road Athlectic Club vs Gokulam Kerala FC | 3.03 | 3.27 | 2.15 |
| 16:00 | 2358 | Wigan U23 vs Millwall U23 | 2.55 | 3.60 | 2.55 |
| 16:00 | 3813 | Crewe U23 vs Bristol City U23 | 4.05 | 3.95 | 1.67 |
| 16:15 | 5767 | Al Jabalain vs AL Draih | 1.44 | 3.72 | 7.34 |
| 16:30 | 4059 | Persepam MU vs Bali Utd Pusam | 5.21 | 3.28 | 1.66 |
| 17:00 | 1305 | Mohammedan SC vs Kenkre FC | 1.09 | 7.69 | 20.19 |
| 17:00 | 1369 | CA Platense vs Gimnasia Y Esgrima La Plata | 2.20 | 3.65 | 2.69 |
| 18:00 | 4905 | FK Panevezys B vs FK Minija | 1.53 | 4.43 | 4.53 |
| 18:30 | 1025 | Al Qadisiyah vs Al Wehda | 1.97 | 3.28 | 3.47 |
| 18:50 | 4140 | AL Akhdood vs AL Kawkab | 2.33 | 2.80 | 3.18 |
| 19:00 | 1097 | Radnik Surduluca vs Partizan | 22.18 | 8.29 | 1.07 |
| 19:00 | 4158 | Adanaspor vs Eyupspor | 2.94 | 3.23 | 2.22 |
| 19:00 | 4949 | Sporting CP U23 vs FC Famalicao U23 | 2.41 | 3.33 | 2.60 |
| 19:00 | 5156 | Concordia Chiajna vs CSA Steaua Bucuresti | 2.85 | 3.00 | 2.41 |
| 19:00 | 5600 | Ferro Carril Oeste vs CA River Plate W | 14.42 | 8.46 | 1.10 |
| 20:00 | 1332 | Siroki Brijeg vs Sloboda Tuzla | 1.80 | 3.08 | 4.53 |
| 20:00 | 1638 | FK Banga B vs Riteriai B | 2.06 | 3.38 | 3.14 |
| 20:00 | 5734 | Flora II vs FCI Levadia Tallinn U21 | 1.62 | 4.46 | 4.36 |
| 20:15 | 1853 | Chojnice vs Ruch Chorzow | 2.13 | 3.17 | 3.17 |
| 21:00 | 1575 | Borussia Dortmund II vs Eintracht Braunschweig | 2.95 | 3.49 | 2.20 |
| 21:00 | 2660 | Cruz Azul W vs Pachucha W | 4.34 | 3.66 | 1.68 |
| 21:00 | 3248 | Hapoel Hadera vs Hapoel Katamon | 2.35 | 2.85 | 3.09 |
| 21:00 | 4181 | Rosario Central vs Club El Porvenir | 1.92 | 3.62 | 3.29 |
| 21:00 | 4392 | Atlas W vs FC Juarez W | 1.22 | 5.62 | 9.69 |
| 21:00 | 5377 | Dunbeholden FC vs Humble Lions FC | 1.96 | 3.19 | 3.62 |
| 21:30 | 2354 | Deportivo Espanol vs Victoriano Arenas | 1.99 | 3.09 | 3.67 |
| 21:30 | 2521 | AS Eupen U21 vs Union Saint Gilloise U21 | 1.68 | 3.96 | 3.96 |
| 21:30 | 2777 | Kortrijk U21 vs Beerschot Wilrijk U21 | 5.18 | 4.61 | 1.45 |
| 21:30 | 4037 | Mouscron U21 vs Oostende U21 | 2.31 | 3.37 | 2.70 |
| 21:30 | 4338 | CS Mioveni vs Chindia Targoviste | 3.04 | 2.79 | 2.55 |
| 21:45 | 3875 | Real Santander vs Leones FC | 2.80 | 3.23 | 2.31 |
| 22:00 | 1514 | Blackburn Rovers U23 vs Derby County U23 | 2.11 | 3.48 | 2.95 |
| 22:00 | 3091 | Stoke City U23 vs Newcastle U23 | 2.01 | 3.37 | 3.28 |
| 22:00 | 3211 | Birmingham U23 vs Norwich U23 | 2.37 | 3.96 | 2.36 |
| 22:00 | 3710 | ADO Den Haag vs Telstar | 1.65 | 3.92 | 4.51 |
| 22:00 | 3898 | West Bromwich U23 vs Nottingham U23 | 2.50 | 3.51 | 2.41 |
| 22:00 | 4363 | Sunderland U23 vs Burnley U23 | 2.80 | 3.53 | 2.17 |
| 22:00 | 5336 | Valerenga W vs Stabaek W | 1.21 | 5.96 | 9.42 |
| 22:00 | 5474 | Pecs MFC vs Kecskemeti TE | 2.51 | 3.09 | 2.65 |
| 22:45 | 4463 | Concarneau vs Chateauroux | 2.09 | 2.98 | 3.67 |
| 22:45 | 5183 | Colchester vs Forest Green | 3.48 | 3.43 | 2.00 |
| 23:00 | 1664 | Cesena vs AC Reggiana | 3.16 | 2.96 | 2.40 |
| 23:00 | 2216 | San Jose FC vs Municipal Garabito | 3.00 | 3.33 | 2.15 |
| 23:00 | 5480 | Tenerife vs Almeria | 2.41 | 3.13 | 2.89 |
| 23:30 | 1590 | Portmore United vs Molynes | 1.70 | 3.86 | 3.96 |
| 23:30 | 1977 | UTC Cajamarca vs Sport Huancayo | 2.33 | 3.14 | 2.85 |
| 23:45 | 2491 | Jaguares de Cordoba vs Union Magdalena SM | 1.53 | 3.58 | 6.00 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Machi 21, 2022

Nipashe




Xavi: Messi anaweza kurudi Barca UKURASA 21

IMEISHA HIYO!...




Mshambuliaji wa Arsenal, Bukayo Saka akishangilia huku akipongezwa na beki wa kulia wa timu hiyo, Cédric Soares (kushoto), baada ya kuifungia timu yake bao pekee wakati ikishinda 1-0 dhidi ya wenyeji, Aston Villa kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa juzi, Jumamosi katika Uwanja wa Villa Park.
**PICHA: MTANDAO**

## Sakho awakuna mashabiki Simba

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI wawakilishi wa pekee wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu, Simba wakiwa wamebakiza mchezo mmoja kukamilisha hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, winga fundi anayetingisha kwa mabao bora kwenye michuano hiyo msimu huu, Pape Sakho, ametoa neno la kukonga nyoyo za mashabiki wa timu hiyo.

Simba jana ilishuka dimbani nchini Benin kuvaana na wenyeji Asec Mimosas ya Ivory Coast, ambayo inachezea mechi zake za nyumbani nchini humo kutokana na viwanja vyao kuwa katika ukarabati mkubwa kwa ajili ya michuano ijayo ya Kombe la Mataifa ya Afrika, Afcon.

Hata hivyo, ukiachana na matokeo ya mechi hiyo iliyopigwa jana usiku, Sakho ambaye anaongoza kwenye michuano hiyo ya CAF kwa mabao yake mawili kuchaguliwa kuwa bora kati ya mechi nne zilizochezwa kwa kila timu kabla ya michezo ya jana, amesema ataendelea kufunga mabao bora iwe za nyumbani ama ugenini.

Sakho ambaye amekuwa gumzo barani Afrika kutokana na mabao yake hayo mawili kuchaguliwa kuwa bora kwenye michuano hiyo, hana hofu kwa timu yake kutinga robo fainali na yeye kuendelea kufunga mabao bora.

"Simba ni timu kubwa na ina kikosi bora, tunaweza kupata pointi tatu katika uwanja wowote ndani na nje ya Afrika," alisema winga huyo raia wa Senegal huku akifunguka kuwa lengo lake ni kuisaidia timu yake kushinda kila mechi.

Simba imebakiza mechi moja ambayo itakuwa nyumbani Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Union Sportive Gendarmerie ya Niger, Aprili 3, mwaka huu.

# Nabi atoa siri Yanga kushinda

**Na Saada Akida**

## ●●● Amshukuru Mayele huku akiipongeza KMC FC na kuishangaa kushindwa kutumia nafasi...

HUKU ikiendelea kukusanya pointi kwenye Ligi Kuu Bara, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amefunguka kwa kutoa siri ya kuendelea kupata matokeo na kukaa kileleni, ambayo ni ngumu kwa sasa timu pinzani kupata dawa ya labda kusubiri hadi dirisha la usajili kufunguliwa na kurejea sokoni kusajili.

**Yanga juzi iliendelea kukusanya pointi baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya KMC FC, kwenye mchezo wa ligi hiyo uliopigwa Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam.**

Kwa matokeo hayo, Yanga ambayo haijawahi kupoteza mechi yoyote kati ya 18 ilizocheza hadi sasa msimu huu, ikishinda 15 na sare tatu, inaendelea kuongoza kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 48 ikifuatiwa na Simba yenye alama 37, lakini ikiwa nyuma mechi moja.

Hata hivyo, akizungumzia baada ya mchezo huo wa juzi, Nabi alisema ulikuwa na ushindani mkubwa, lakini ukubwa wa wachezaji wake umewanufaisha kupata matokeo mazuri na kuendelea kupata pointi tatu.

Alisema siri kubwa ya timu yake kupata matokeo kwenye mechi za ligi hiyo pamoja na mambo mengine, lakini kubwa ni kutokana na kikosi chake kujengwa na wachezaji wakubwa ambao wanajua nini cha kufanya wanapokuwa uwanjani kutafuta alama tatu.

Alisema katika kipindi cha kwanza wachezaji hawakucheza kama alivyowaelekeza, lakini KMC FC walikuwa bora kwa kutengeneza nafasi nyingi za wazi na kushindwa kuzitumia.

"Wapinzani walicheza kwa nidhamu kubwa, walikaba kwa pamoja hali ambayo wachezaji wangu hawakutegemea na kutocheza kwa maagizo niliyowapa.

"Niwapongeze KMC kwa kucheza vizuri na walishindwa tu kuzitumia nafasi walizotengeneza, lakini kipindi cha pili tuliweza kubadilisha mchezo na kushinda," alisema na kuongeza:

"Nawashukuru Mayele (Fiston) na Shaban (Djuma), kuweza kutumia nafasi tulizopata na kufunga mabao hayo, yaliyotupatia ushindi na kuendelea kuongoza ligi."

Katika mechi hiyo mabao yalifungwa na beki wa KMC, Andrew Vincent 'Dante' aliyejifunga dakika ya 39 kipindi cha kwanza katika harakati za kuokoa mpira uliounganishwa na Mayele huku lile la pili likizamishwa nyavuni kwa kichwa dakika ya 52 na beki Mkongo Djuma Shaaban.

Naye Kocha Mkuu wa KMC FC, Thierry Hitimana, alisema wanatatizo katika safu ya ulinzi licha ya kufaulu kipindi cha kwanza kwa kuwazuia Yanga kupata bao kabla ya Dante kujifunga dakika sita kabla ya kwenda mapumziko.

"Tumekubali matokeo na kulingana na mchezo ulivyokuwa, nakiri kwamba nina mapungufu ya safu yangu ya ulinzi, tunaendelea kufanyia kazi, lakini pia tunatakiwa baada ya ligi kulifanyia kazi hilo," alisema Hitimana.

Alisema walitengeneza nafasi nyingi, lakini wachezaji hawakuwa makini kuzitumia na sasa wanajipanga kwa ajili ya michezo yao ijayo.

KMC inasalia nafasi ya saba kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama zake 22 baada ya kushinda michezo mitano, sare saba na kupoteza sita kati ya 18 ambayo imeshacheza hadi sasa.

Ligi hiyo kwa sasa imekwenda mapumziko kupisha mechi za Kalenda ya Fifa, na itakaporejea, Aprili 3, KMC itaikaribisha Namungo FC wakati Yanga itakuwa ugenini kuvaana na Azam FC katika mchezo utakaopigwa Aprili 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >